# Nipashe

Jumatatu Mei 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581304

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


MID WEEK JACKPOT!

TZS. 575,472,890

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Vipimo vya DNA mtoto 'aliyefufuka' vyaibua mapya

UKURASA 3

# Kumekucha Katiba mpya



• **Rais** Samia apuliza kipenga, wadau... *Endelea Ukurasa 3*




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipokea zawadi ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoka kwa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, wakati wa ibada ya kuwekwa wakfu na kuingizwa kazini Askofu Mteule Christian Ndossa na msaidizi wake, Mch. Stanley Tabulu, iliyofanyika katika Kanisa la KKKT Dayosisi ya Dodoma jana. **PICHA: OMR**

UFISADI SERIKALINI

## Askofu Shoo atoa angalizo ubadhirifu mali za umma

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### MCHUNGAJI AONA UKAKASI MASHOGA KUPELEKWA JELA

MCHUNGAJI wa Kanisa la Moravian Usharika wa Singida Mjini, Yona Mbogo ameonya kuwa kuwakamata na kuwaweka gerezani kwa pamoja wanaojihusisha na vitendo hivyo ni kuongeza ukubwa wa tatizo...

UKURASA WA 9

### TISHIO LA UMWAGAJI DAMU LAMSHTUA DC

TISHIO la umwagaji damu lililotolewa na familia mbili za kifugaji katika Kijiji cha Lendikinya, Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, limemshtua Mkuu wa Wilaya hiyo...

## Unywaji pombe kuponza watumishi wa DART

UKURASA 8






Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Seleman Jafo, akinunua viatu pamoja mikoba baada ya kuzindua kiwanda kidogo cha kutengeneza bidhaa za ngozi wilayani Kishapu juzi wakati wa ziara yake ya kukagua, kuweka jiwe la msingi na kuzindua baadhi ya miradi ambayo inatekelezwa wilayani humo ya kuhimili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: MARCO MADUHU**

UFISADI SERIKALINI

# Askofu Shoo atoa angalizo ubadhirifu mali za umma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, ameishauri serikali kushughulikia kwa ukali tuhuma za ubadhirifu zinazosikika kuiandama miradi mikubwa yenye manufaa kwa taifa.

Askofu Shoo pia amesema kanisa hilo haliungi mkono vitendo vya ushoga na ndoa za jinsia moja na halitoacha kutumia rangi za upinde wa mvua kwenye nembo yake kwa kuwa "ni agano la Mungu".

Akizungumza jana kwenye ibada ya kuwekwa Askofu wa KKKT Dayosisi ya Dodoma, Christian Ndossa, Askofu Shoo alisema: "Ninaipongeza serikali kwa miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa kwa sasa.

"Ni imani yetu na matumaini yetu na tunaombea miradi isimamiwe vizuri na kukamilika kwa wakati na ikiwa hivyo, miradi itakuwa na manufaa makubwa kwa taifa hili na mataifa jirani.

"Jambo kubwa tunaloomba - shughulikieni kwa ukali sana tuhuma za ubadhirifu tunazozisikia zinazoanza kuandama miradi hii mikubwa na kwa manufaa ya taifa letu. Shughulikieni kwa ukali na kwa maneno," alisema.

Askofu Shoo alisema miradi na mipango mingine ya maendeleo zikiwamo hudumu za kijamii, ikiendelea kuzungukwa na tuhuma za ubadhirifu na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za ununuzi, badala ya kuleta furaha na shangwe, itasababisha sintofahamu na kunyong'onyesha wananchi.

"Huku ni kukosa uzalendo. Ni kuliua taifa letu. Kuwaumiza walipakodi ambao kimsingi fedha inayoendesha miradi hii na huduma hizi ni kodi wanazotozwa wao.

"Ni vyema kodi za watu maskini kama ilivyo nchi yetu zisimamiwe na kutumika vizuri kwa ajili ya kuleta maendeleo wananchi walio wengi kuliko kuwafaidisha watu wachache wabinafsi, walafi, ambao mimi ninasema kimsingi wanaliangamiza taifa letu.

"Watu ambao ukiwaangalia kwenye maisha yao, mishahara yao, vipato vyao wana hali nzuri. Sasa kwanini watumie nafasi zao kuwaumiza na kuzuia kile kinachokwenda kumsaidia yule wa hali ya chini? Tunahitaji kuhimiza uzalendo, uadilifu na uamininifu na hizi ndizo zikawe tunu na alama za viongozi bora wa taifa letu na ndio tunaowataka," alisema.

**UPINDE WA MVUA**

Askofu Shoo pia alikemea vikali upotoshaji kwa kuhusisha nembo ya KKKT na masuala ya mapenzi ya jinsia moja na kuwataka wanaotumia alama hizo kwa matendo yasiyofaa wakemewe.

"Hii nembo katikati ina ua ambalo ilibuniwa na Martin Luther. Ijulikane wazi kuna watu kwa kutofahamu eti kwa sababu siku hizi limetokea kundi la washenzi, wapumbavu, wanatumia alama za upinde wa mvua kama alama yao, leo hii ambao tunafahamu historia na kiini na maana ya rangi za upinde wa mvua leo eti tuogope tusitumie alama hizo.

"Katika kitabu cha Mwanzo rangi za upinde wa mvua ni agano la Mungu na wanadamu aliloweka. Halafu leo kitokee kikundi cha wahuni waseme hii ni alama yetu halafu sisi tuseme hii alama tusiitumie tena. Upinde wa mvua ni alama ya Mungu tangu wakati wa Nuhu," alisema.

Askofu Dk. Shoo alisema kanisa halipaswi kuogopa kutumia rangi za upinde wa mvua, bali ni wajibu wao kuwaambia watu wanaotumia visivyo kuacha kutumia rangi hizo.

"Tusipowakemea kesho litazuka lingine watatumia msalaba. Watasema 'sisi ni kundi la wale watu na ndio alama yetu', lazima tulinde alama zetu za kiimani na wahuni waache kutumia alama zetu na huu ndio msimamo wetu," alisema.

Kiongozi huyo wa kanisa pia alisisitiza msimamo wao kutounga mkono mapenzi ya jinsia moja, akisema: "Siku za hivi karibuni jambo la ushoga na ndoa za jinsia moja limeshamiri sana. Lazima kila mmoja wetu ajiulize kwanini? Ninakupongeza Makamu wa Rais (Dk. [Phillip Mpango) kwa kauli uliyotoa kukemea jambo hili lakini pia nipongeze serikali kwa kuweka wazi kuwa jambo hili halikubaliki hata kidogo hapa kwetu.

"Tunahitaji kuwa macho kwelikweli na kuchukua hatua zote za kupinga, kukemea na kukataa jambo hili. Tuungane sote katika kuimarisha malezi bora. Kuna wakati nilisema inawezekana sasa hivi tunacheza na matunda, matokeo ya kutozingatia malezi bora, kuwalea watoto katika njia iwafaayo," alisema.

Askofu Shoo alibainisha kuwa hali si nzuri vyuo vikuu, akirejea taarifa kutoka kwa baadhi ya wazazi wanaowafikia viongozi wa dini wanalia hawajui kilichotokea kwa vijana wao. Wamebadilika!

"Tunahitaji kuomba sana kutoa ushauri na nasaha kwa wale waliokumbwa na hali hii wanateseka hawajui watokaje. Ndugu zangu tusiache mafundisho na imani sahihi kwa kuwa mimi ninaamini hapa ndio chanzo cha kuporomoka. Wanasema dunia ikimwacha Mungu. Dunia inaanza kulewa na kuwayawaya kama mlevi."

Kuhusu uhifadhi wa mazingira, Askofu Shoo alisema kunahitajika nguvu ya kutosha na mipango endelevu ya utunzaji mazingira kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Athari ni kubwa sana. Tunaisihi serikali kulitazama hili kwa jicho la kipekee sana. Viongozi wa dini na wadau wengine tukaweke mkazo sana, vinginevyo tutakuwa tunaangamiza kizazi chetu wenyewe. Kuharibu mazingira ni kuandaa mpango wa kifo kwa vizazi vyetu," alionya.

# ...Mpango ataka viongozi wa dini kukemea ufisadi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka viongozi wa dini kuendelea kukemea ubadhirifu wa mali na fedha za umma, akisisitiza kuwa wanaotenda hayo ni waumini wa madhehebu ya dini.

Pia ameonywa kuwa Ukimwi bado upo huku akieleza kushangazwa na wanaokwenda saluni usiku wa manane kufanyiwa 'massage'.

Dk. Mpango akizungumza jana kwenye ibada ya kuwekwa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Christian Ndossa, alisema viongozi hao waendelee kupaza sauti za ubadhirifu na serikali inazifanyia kazi tuhuma za ubadhirifu katika miradi ya kimkakati na ikithibitika itachukua hatua kali.

"Ninyi viongozi wa dini endeleeni kupaza sauti zenu za mamlaka ya kimungu dhidi ya ubadhirifu serikalini na katika taasisi za kidini kwa kuwa baadhi ya mafisadi ni waumini wa dini zetu," alisema.

Dk. Mpango alisema viongozi hao wahimize Watanzania kufanya kazi na si kupata mali na fedha kwa njia zisizo halali au ujanja, kukemea ubadhirifu na rushwa, kuhimiza uzalendo, utu mwema na kutunza mazingira.

Aliomba madhehebu ya dini kusimama katika nafasi yake ya kufundisha, kuonya na kukemea kwa nguvu matendo yasiyofaa bila kukata tamaa kwa kuwa serikali inawategemea.

Dk. Mpango alisema athari za mmomonyoko wa maadili zinaonekana kwa viongozi na baadhi ya waumini wa madhehebu ya dini kwa kwenda kinyume cha maandiko ya Mungu.

"Kumekuwapo na viongozi wachache wa dini wanaoharibu taswira ya dini kwa njia ya mafundisho na mienendo isiyofaa kwa jamii. Bado tunashuhudia migogoro ndani ya makanisa na misikiti.

"Mtakumbuka hivi karibuni nchi jirani mtu mmoja amewafungisha watu. Wanakufa kwa wingi, jambo la kusikitisha kabisa! Ninaendelea kuwasisitiza viongozi wa dini mjitahidi kumaliza tofauti zenu ninyi wenyewe kabla ya kufikishana mahakamani," alisema.

**SALUNI USIKU MNENE**

Makamu wa Rais alisema Ukimwi bado upo, lakini watu wamejisahau na kuomba viongozi wa dini kuendelea kupaza sauti.

"Kuna mambo yanasikitisha. Hata saluni watu wanakwenda usiku wa manani. Sijui wanakwenda kufanya nini. Kuna vitu vingine vinaitwa massage, saa saba usiku? Yote hayo ni matumizi mabaya na mianya ya kufanya uovu. Serikali itafanyia kazi," alisema.

Dk. Mpango pia alisema kumekuwa na wimbi la kesi za talaka na wajane na yatima kunyang'anywa mali zilizoachwa na wenza au wazazi kinyume cha mafundisho ya dini.

"Familia nyingi zinaathirika na kuacha kinamama na watoto wakiteseka. Mmomonyoko wa maadili tunaoshuhudia unachangiwa na malezi mabaya, kuvunjika kwa ndoa, matumizi holela ya mitandao ya kijamii. Mpango wa dini watoto walelewe na kufundishwa maadili mema," alisema.

Aliomba viongozi wa dini kusaidia kumaliza migogoro ya ndoa na mirathi kwa amani na utii kwa Mungu.

Dk. Mpango pia alizungumzia athari za mabadiliko ya tabianchi, akionya: "Uharibifu mkubwa umeendelea kusababisha maafa makubwa duniani na nchini kwetu. Kwa mujibu wa taarifa ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2022, inakadiriwa watu milioni 700 duniani wako katika hatari ya kuhama makazi yao itakapofika mwaka 2030 kwa sababu ya ukame.

"Takribani watu bilioni tatu hadi 3.6 wanaishi katika mazingira yenye uwezekano wa kukabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kuongezeka kwa joto duniani kunatarajia kuongeza kina cha bahari na kuathiri maisha ya watu wanaoishi kwenye visiwa na kando ya bahari," alisema.

Alirejea ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) inayobainisha kuwa mabadiliko ya tabianchi yatasababisha ongezeko la vifo 250,000 duniani kati ya mwaka 2030 na 2050.

"Niwakumbushe waumini tusipotunza mazingira yetu, tutajiangamiza wenyewe. Wengi ni mashahidi mafuriko ya hivi karibuni Arusha, tunashuhudia ukame na uharibifu mkubwa wa mazingira, vifo vya mifugo, miaka si mingi iliyopita mazingira hayakuwa hivi kama leo," alisema.

Makamu wa Rais pia aliwahimiza viongozi wa KKKT kutunza mali za kanisa kiadilifu, kuepuka tamaa za mali na vyeo na waumini wasiwe wachochezi wa migogoro ya kanisa.

# Kumekucha Katiba mpya

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kuitisha kikao maalum cha Baraza la Vyama vya Siasa, ili kuwashirikisha wadau kufanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi kilichoratibu maoni ya watu kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini.

Katika taarifa yake juzi usiku, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Zuhura Yunus, alisema Rais Samia alitoa maelekezo hayo wakati wa kikao kilichofanyika Ikulu, Chamwino, kilichohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali kuhusu kuanza kwa mchakato wa Katiba mpya.

Kwa mujibu wa Zuhura, kikao hicho kilijadili namna ya kushirikisha wadau mbalimbali na hasa ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa Katiba mpya kutoka pande zote mbili - Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Alisema mbali na mchakato huo wa Katiba mpya, masuala mengine yanayotarajiwa kushughulikiwa ni marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusiana na uchaguzi; zikiwamo Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa. Vipaumbele vingine ni pamoja na maboresho ya sheria za uchaguzi kuelekea uchaguzi ujazo mwaka 2024 wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025 wa madiwani, ubunge na urais.

Katika kikao cha Rais Samia na viongozi hao wa serikali, walijadili ushirikishwaji wa wadau mbalimbali na hasa wananchi kwenye mchakato huo wa Katiba.

Viongozi waliohudhuria kikao hicho ni pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Jenista Mhagama, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro na watendaji wa taasisi mbalimbali.

Maagizo hayo ya Rais Samia yametolewa ikiwa ni wiki chache zimepita tangu Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro awasilishe bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, vipaumbele vyake ikiwa ni kuukwamua mchakato wa Katiba mpya uliokwama.

Kikosi kazi hicho kilichokuwa kikiongozwa na Mwenyekiti, Prof. Rwekaza Mukandala pamoja na mambo mengine, kilipendekeza mchakato wa Katiba mpya uliokwama mwaka 2014 kwa hatua ya Katiba Pendekezwa, ufufuliwe.

**ACT YAUNGA MKONO**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa umma na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, chama hicho kinaunga mkono na kuikaribisha kwa mikono miwili hatua ya Rais Samia kumwagiza Msajili kukutana na Baraza la Vyama vya Siasa.

"Imekuwa ni rai ya mara kwa mara ya ACT -Wazalendo kuhitaji ratiba ya utekelezaji wa mapendekezo ya kikosi kazi. Ni matumaini yetu kuwa kikao hicho kitapatiwa ratiba hiyo ambayo itahakikisha tuna Sheria mpya ya Uchaguzi na Sheria mpya ya Vyama vya Siasa kabla ya mwisho wa mwaka huu.

"Ni matarajio ya chama chetu kuwa Baraza la Vyama vya Siasa litakuwa ni sehemu ya mandalizi ya mkutano wa kitaifa, ili kujadili mambo yaliyokwamisha mchakato wa Katiba mwaka 2014 na kupata mwafaka kwao ili mchakato wa sasa usikwame," alisisitiza.

# Vipimo DNA mtoto 'aliyefufuka', kuokotwa porini vyaibua mapya

**Na Vitus Audax,** MWANZA

VIPIMO vya vinasaba (DNA) vya mwili wa mtoto Mabirika Wilson (8), aliyefariki dunia Aprili 16 mwaka huu wilayani Magu, pamoja vya wazazi wake, vimeonyesha ni mtoto wao.

Uchunguzi huo unapingana na madai ya awali kwamba mtoto huyo amekutwa akiwa hai katika wilaya nyingine ya Kwimba mkoani hapo.

Vipimo hivyo vilivyofanywa na wataalamu wa afya kutoka Kitengo cha 'Forensic' wakishirikiana na wataalamu kutoka Ofisi ya Mkemia wa Serikali baada ya kupata kibali cha kufukua mwili na kuufanyia vipimo kutoka mahakamani, vimeonesha kuwa mtoto aliyeokotwa wilayani Kwimba Aprili 27 hana uhusiano na wazazi hao, hivyo mtoto wao halisi ni yule aliyeugua na kufariki dunia Aprili 16, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, aliyesema kuwa baada ya kubaini ukweli huyo, jeshi linawashikilia wazazi wa mtoto huyo ambao ni Wilson Bulabo (35) na Helena Robert (33) kwa kufanya udanganyifu na kuzua taharuki katika jamii, wakitaka kujipatia mtoto aliyeokotwa ilhali siyo mtoto wao.

"Haiwezekani kwa kipindi cha siku 10 tu wazazi wawe tayari wamemsahau mtoto wao ambaye wamekaa naye kwa kipindi cha miaka minane na kuanza kumfananisha na mtoto ambaye sio wao.

"Hivyo, baada ya uchunguzi wa kina kufanyika, watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuzua taharuki katika jamii na kuaminisha watu juu ya ufufuko wa mtoto wao," alisema Kamanda Mutafungwa.

Kamanda huyo alisema kuwa baada ya mtoto huyo kuhojiwa katika hali ya utulivu, alijitambulisha kwa jina moja la Mussa, hivyo kuwataka wazazi ambao watakuwa walipotelewa na mtoto kufika kituoni huko kumtambua kwa kuwa kwa sasa anahifadhiwa katika moja ya kituo cha kulelea watoto ambacho hakuwa tayari kukiweka wazi kwa sababu za kiuchunguzi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwangika, Jeremaniuss Masala, alisema kuwa baada ya kumpata mtoto huyo, walitangaza ili kuwapata ndugu zake na walipotokea wazazi hao na kueleza juu ya mtoto wao kufariki dunia na kudai huyo ndiye mtoto aliyefariki, wakaamua kushirikisha vyombo vya sheria kuondoa utata huo ambao ungesababisha madhara kutokana na kuhusishwa na ushirikina.

**JARIBIO KUJIUA**

Kamanda Mutafungwa pia alitangaza tukio la mwanamume anayeitwa Marco Samwel (32), aliyekita na kuondoa kabisa uume wake akiwa na lengo la kujiua kutokana na kuugua kwa muda mrefu bila kupona.

Alisema kuwa mtu huyo anaendelea kupatiwa matibabu na anaendelea vizuri chini ya ulinzi wa polisi na pindi akipona, atafikishwa mahakamani kwa kosa la kujijeruhi.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA KUHUDUMA YA BIMA YA DHIMA KWA WAKURUGENZI NA MAAFISA WA EACOP KUMBUKUMBU NA. REQ-00000195

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ("EACOP LTD") inakaribisha kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya Bima ya Dhima kwa wakurugenzi na Maafisa wa Mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unajumuisha shughuli za ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafutaghafi lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili kwa ajili ya kusafirisha Mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa waTanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU HUDUMA**

EACOP inahitaji kupewa huduma ya Bima ya Dhima kwa wakurugezi na Maafisa wake. Lengo la maombi haya ya kuonesha ni kukaribisha kampuni za Bima kutoa huduma ya Bimaya dhima kwa wakurugenzi na maofisa (ikijumuisha mameneja na wasimamizi) ("D&Os") wa EACOP. Huduma ya Bima iwe na uwezo wa kupatikana duniani kote na ikijumuisha pamoja na mambo mengine.

1. Madai yoyote yanayotokana na/au tukio wakati wa utendaji kazi wa Wakurugenzi na Maafisa wengine wa EACOP. Madai yatakayotambulika ni yale yanayojumuisha madai yoyote ya maandishi au kesi za kudai fidia au fidia zozote za kisheria ikiwa ni pamoja na kesi za jinai na uchunguzi rasmi.
2. Madai yanayohusiana na athari za kimazingira, kijamii na kiutawala.
3. Gharama za utetezi wa kisheria, gharama za fidia, gharama za mahusiano ya kijamii, madhara ya kiutawala, ulinzi wa wakurugenzi wasio watendaji, gharama yingine za lazima zisizo za kila mara, gharama za dharura, elimu ya mazingira, vifo vinavyoihusisha kampuni, gharama za nje ya shughuli za ukurugenzi, kesi za kuondolewa nchini, gharama uchunguzi, malipo ya uzeeni kwa watumishi wastafu waliokuwa wanufaika wa bima, kampuni tanzu mpya, nyongeza ya muda wa uwakilishi kisheria, ongezeko la kodi, dhima ya mali ya pamoja.
4. Uharibifu na tozo au faini (kama zina bima) zinazowakabiili wajumbe wa bodi, wakurugenzi, na menejimenti ya EACOP endapo madai ya kisheria yatatolewa.
5. Pamoja na maeneo mengine ya wigo wa bima husika kadri ambavyo kwa kawaida huhitajika kwa wakurugenzi na maafisa wa kampuni.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo**

- Kampuni iwe imesajiliwa na kuruhusiwa kufanya kazi nchini Uganda na Tanzania.
- Kampuni iwe ina uzoefu wa kutoa huduma ya bima ya dhima kwa wakurugenzi na maafisa kwa muda usiopungua miaka mitano. Ikijumuisha uzoefu wa kutoa bima ya dhima kwa wakurugenzi na maafisa angalau kwa kampuni moja ya kimataifa.
- Iwe na bima ya kiwango cha makadirio ya A – au zaidi cha nguvu ya kiuchumi kulingana na makadirio ya wakala wa makadirio anayeaminika.
- Kampuni lazima ioneshe rekodi inayothibitika ya kulipa madai ya bima kwa haki na kwa haraka.
- Uthibitisho wa barua kutoka walau makampuni au mashirika matatu (3) zikionesha mhusika mkuu ambaye amewahi kupata huduma kama hiyo toka kwenye kampuni husika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka miwili iliyopita.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa au wana uthibitisho wa maombi yaliyoidhinishwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia, Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Mlipa kodi cha mwaka wa hivi karibuni Leseni halali ya kitaaluma, kutoka mamlaka ya ndani ya nchi husika kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe **21 Mei 2023 saa 10 jioni** saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000195 - kutoa huduma ya Bima ya Dhima kwa wakurugenzi na Mafisa wa Mradi wa EACOP**. Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20 Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# CRDB, Care International kuwainua wanawake kupitia programu IMBEJU

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetia saini makubaliano ya kushirikiana na Shirika la Care International kuwawezesha wanawake kupata mafunzo ya namna bora ya uendeshaji wa biashara, usimamizi wa fedha na mitaji pamoja na kuwapatia mitaji wezeshi ya kujikwamua kiuchumi kupitia programu ya IMBEJU.

Akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini makubaliano hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, amesema taasisi hiyo inafurahia kuingia mkataba wa ushirikiano na Shirika la Care International kwani utakwenda kuwezesha programu ya IMBEJU kuwafikia wanawake wajasiriamali wengi zaidi nchini.

Tully alisema lengo ya programu ya IMBEJU ni kuongeza ujumuishi wa kiuchumi nchini, hivyo ushirikiano na Care International unakwenda kusaidia kufikia lengo hilo kwa kuwa shirika hilo limekuwa linajihusisha na uwezeshaji wa vikundi vya kiuchumi kote nchini kwa takribani miongo mitatu.

Tully aliwakaribisha wabia wengine wa maendeleo nchini kushirikiana katika programu hiyo ya IMBEJU ili kuleta matokeo chanya zaidi na kuwezesha makundi ya vijana na wanawake.

"Benki yetu na taasisi yetu ya CRDB Bank Foundation inaamini katika ubia kama msingi wa kutatua changamoto zilizopo katika jamii yetu. Niwashukuru Care International kwa utayari wao wa kushirikiana nasi kupitia programu ya wanawake. Tunawakaribisha na wadau wengine waje tuunganishe nguvu," alisema.

Aliishukuru serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Tume ya TEHAMA (ICTC) kwa ushirikiano ambao inautoa kupitia programu ya biashara changa bunifu za vijana.

Hivi karibuni Benki ya CRDB ilitangaza matokeo ya programu shindani ya vijana ambapo vijana 706 waliwasilisha maombi huku 106 wakichaguliwa kushiriki mafunzo kabla ya kupewa mitaji wezeshi.

"Programu ya wanawake kupitia IMBEJU bado dirisha lake lipo wazi, na tumeendelea kuongeza nguvu kwa kushirikiana na Care International ili tuwafikie wengi zaidi. Nitoe rai kwa wanawake wajasiriamali kuchangamkia fursa hii ili kuboresha shughuli zao," aliongezea Tully akitoa hamasa kwa wanawake.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Care International, Prudence Masako, alisema CRDB Bank Foundation ni mbia muhimu kwao kwani juhudi zao za kukabiliana na umasikini zitafanikiwa kutokana na uhakika wa fedha za uwezeshaji kupitia programu ya IMBEJU.

Mkurugenzi huyo alisema Care International ilianzishwa miaka 78 iliyopita lakini ina miaka 29 tangu liingie nchini na katika mkakati wake wa kusaidia jamii kupambana na umaskini, inafanya kazi na vikundi zaidi ya 50 vyenye wanachama wasiopungua 600,000.

"Moja ya malengo makuu ya Care International ni kusaidia jitihada za kupunguza umaskini. Hivyo, tuliposikia kuhusu programu ya IMBEJU tulifurahi kwani hii ni fursa ya kuwafikia watu wengi ambao wameachwa nyuma katika shughuli za kiuchumi.

"Vilevile, tunaamini katika usawa, hakuna jamii imeendelea kama mwanamke hajaendelea," alisema Prudence huku akiwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kushiriki programu ya IMBEJU.

Kunufaika na uwezeshaji kupitia programu ya IMBEJU, wanawake wanatakiwa kuwa katika vikundi na kisha kuwasilishwa maombi kupitia tawi lolote la Benki ya CRDB nchini, au kupitia mfumo wa uwezeshaji wa vikundi wa Care International.

Vikundi vitatakiwa kutia saini makubaliano ya kushiriki programu ya IMBEJU, na kisha kupatiwa mafunzo na Shirika la Care International au maofisa uweshaji wa CRDB Bank Foundation. Mitaji wezeshi inatolewa kwa mwanachama mmoja mmoja wa vikundi baada ya kuhitimu mafunzo.

Programu ya IMBEJU ilizinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Machi 12, mwaka huu na kufungua dirisha la ufadhili kwa biashara changa za vijana na wanawake wajasiriamali. Zaidi ya Sh. bilioni tano zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake kupata mtaji wezeshi wa kuendesha biashara zao kupitia programu hiyo.




Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa (kulia), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla fupi ya kusaini mkataba wa ushirikiano katika ya taasisi hizo kupitia programu ya IMBEJU unaolenga kuwawezesha wanawake wajasiriamali wengi zaidi kote nchini kupitia mafunzo na mitaji wezeshi iliyofanyika mwishoni mwa wiki makao makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam. Wengine ni Mkurugenzi Mkazi wa Care International, Prudence Masako (katikati) na Mkurugenzi wa Miradi Care International, Haika Mtui. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kortini madai kughushi na kujipatia milioni 20/-

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Yusuph Muhamed Abdul Aziz, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, akikabiliwa na mashtaka matatu, likiwamo la kughushi na wizi wa Sh. milioni 20, mali ya Kampuni ya Cozy Traders (T) Ltd.

Akisoma hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka, Agatha Lumato, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Ilala, Aneth Myenyemi, alidai mshtakiwa alitenda makosa hayo Mei mwaka jana.

Katika shtaka la kwanza, ilidaiwa kuwa Mei 22, 2022, ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, kwa nia ovu mshtakiwa alitoa azimio maalum la uongo la Mei 22, 2022 likionyesha kuwa ni hati halisi iliyotolewa na wakurugenzi wa Kampuni ya Cozy Traders (T) Ltd huku akijua sio kweli.

Alidai katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Mei 22, 2022, ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa kwa kujua na kwa udanganyifu, alitoa hati ya azimio la kughushi akionyesha kuwa ni hati ya kweli wakati sio kweli.

Lumato alidai mahakamani kuwa, katika shtaka la tatu, mnamo Juni 8, 2021, ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa aliiba Sh. milioni 20 kutoka kampuni ya Cozy.

Baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka hayo, alikana kuhusika na tuhuma hizo. Upande wa mashtaka ulidai upelelezi umekamilika na kesi imeahirishwa hadi Juni 06, mwaka huu.

# Polisi yaonywa rushwa ya kuwezesha dhamana

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Geita, Safia Jongo, amewaonya askari polisi kuchukua fedha kwa watuhumiwa wa makosa mbalÅimbali kwa madai ya kuwezesha upatikanaji wa dhamana, watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Jongo alitoa onyo hilo jana alipozungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa Zahanati ya Kijiji cha Rwamgasa wilayani Geita mkoani hapa.

"Wakati wa utawala wangu mkoani Geita, sitaki kusikia askari polisi wanachukua fedha kwa ajili ya dhamana. Dhamana ni haki ya mtu na inatolewa bure. Mimi ninataka mtu akiingia polisi bure na kutoka bure. Yeyote atakayeombwa fedha, awasiliane nami muda wowote," alisema.

Kamanda Jongo alitoa agizo hilo baada ya wananchi wa Kijiji cha Rwamgasa waliokuwa kwenye mkutano huo wa hadhara, kulalamika wanapokwenda kuwadhamini ndugu zao kwenye vituo vya polisi, wanadaiwa fedha ndipo wapewe dhamana.

Kamanda Jongo pia aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi ikiwamo kuua wazazi wao kwa lengo la kujipatia mali au kuwahusisha na imani za kishirikina.

Alisema kama kuna mtu yeyote wanayehisi ni mchawi, watoe taarifa kituo cha polisi, ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mtu huyo kuliko kujichukulia sheria mkononi.

Pia aliwataka wananchi wa kijiji hicho kutoa taarifa kituo cha polisi wanapoona ukatili kwa watoto na wanawake, ili sheria ichukue mkondo wake na kupunguza vitendo vya kikatili.

Aliwataka waganga wa kienyeji wanaojihusisha na tabia za udanganyifu na uchonganishi kwa jamii kuacha mara moja kwa kuwa watakaobainika, watachukuliwa hatua za kisheria.

TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Yanga mna nafasi ya kuitoa Marumo

**TIMU** ya Yanga keshokutwa Jumatano inashuka dimbani kucheza na Marumo Gallants ya Afrika Kusini kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, CAF.

Mchezo huo utapigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam na marudio ni Mei 17 nchini Afrika Kusini.

Yanga imetinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kuitoa Rivers United ya Nigeria kwa jumla ya mabao 2-0. Yanga ilianza kwa ushindi wa 2-0 ugenini na baadaye suluhu kwenye dimba la Mkapa.

Matokeo hayo yakaifanya Yanga isonge mbele na kujiwekea historia yake ya kutinga kwa mara ya kwanza hatua ya nusu fainali ya kombe hilo na sasa ina kibarua cha kuivaa Marumo.

Yanga ambayo kwa sasa inaongoza msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na ikiwa inahitaji pointi tatu tu kutangazwa kuwa mabingwa wapya, tunaamini kwamba wana kikosi kizuri chenye uwezo wa kuitoa Marumo na kutinga fainali.

Tunasema hivi kwa sababu ya ubora wa kikosi chenyewe cha Yanga ambacho kinanolewa na Kocha Nasreddine Nabi raia wa Tunisia akisaidiwa na Cedric Kaze, huku pia wakiwa wametinga nusu fainali nyingine ya Kombe la Shirikisho Tanzania (FA).

Tunafahamu kwamba, Yanga imefika hatua hiyo kutokana na kujituma kwa wachezaji wake, pamoja na ubora wa benchi lake la ufundi, hivyo tunaamini kabisa sasa ni wakati wa kuonesha kiwango kingine bora zaidi kwenye hatua hiyo.

Wapinzani wao Marumo hivi sasa wanapigania kutoshuka daraja kwenye Ligi Kuu ya nchini kwao Afrika Kusini na mwishoni mwa wiki (Jumamosi), walikutana na kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Mamelod Sundown, hivyo Yanga wakitumia udhaifu wa timu hiyo vizuri wana nafasi kubwa ya kuwatoa na kutinga fainali. Tunaamini kwamba, timu yoyote inapocheza kwenye dimba lake la nyumbani ina nafasi nzuri zaidi ya kupata matokeo chanya na hivyo kujiweka kwenye wakati mzuri zaidi katika mchezo wa marudiano ugenini.

Hivyo Yanga inapaswa kutumia vizuri uwanja wa nyumbani wa Mkapa kuhakikisha inaibuka na ushindi wa mabao mengi, ili kurahisisha kazi kwenye mchezo wa marudiano.

Iwapo Yanga itapata ushindi wa mabao mengi itakuwa imejirahisishia kazi kuelekea mchezo wa marudiano, kwa sababu kazi kubwa watakayokuwa nayo ni kupambana kupata sare yoyote ili kutinga fainali.

Hata hivyo, pamoja na kwamba, wapinzani wao Marumo wanapambania kutoshuka daraja kwenye Ligi Kuu ya nyumbani kwako Afrika Kusini (ipo nafasi ya 14 katika timu 16 na pointi 29), lakini Yanga hawapaswi kuwabeza hata kidogo.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba, licha ya kuwa na matokeo mabaya kwenye ligi ya nyumbani, lakini Marumo imeoneshwa kiwango bora na cha kuvutia kwenye michuano hii ya Shirikisho.


Ikimbukwe kwamba, Marumo hawa waliwalazimisha sare ya kufungana bao 1-1 na Pyramids ya Misri ugenini kabla ya kushinda bao 1-0 nyumbani na kutinga hatua hiyo iliyopo sasa.

Hivyo basi, Yanga wanatakiwa kuingia kwenye mchezo huo kwa tahadhari kubwa sana, kwani wapinzani wao hawatabiriki, masihara au umakini mdogo unaweza kuwafanya wawe na wakati mgumu.

Tunaamini benchi la ufundi la Yanga limeifuatilia kwa ukaribu na umakini mkubwa michezo yote ya Marumo na kwamba hivi sasa wanajua ubora na udhaifu wa kikosi hicho.

Sisi Nipashe tukiwa kama mdau namba moja wa mchezo wa soka la michezo yote kwa ujumla, tuna imaini kubwa na Yanga na hivyo tunawatakia kila la heri kwenye mchezo wao huo na tunaamini hawatawaangusha Watanzania kwa sababu wanaliwakilisha Taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Wanahabari wasiache upotoshwaji historia ya soka

**WAKATI** tunasoma shule kuanzia shule ya msingi hadi sekondari, tumefundishwa vitu vingi ikiwamo historia za mashujaa wetu, kuna Mtemi Milambo, Mkwawa, Pazi, Songea Mbano, Kinjekitile na wengine wengi.

Hatukuwaona, lakini tumesimuliwa na kufundishwa na tumeendelea kuwaimba na kuwaandika kama mashujaa. Hakuna hata mmoja kati yetu aliyeonyesha kuwa na shaka kama Mkwawa kweli aliwakong'ota Wajerumani.

Kuna kikundi cha watu kwa makusudi, wameamua kupotosha historia na rekodi za soka, na wamekuwa wakisapotiwa na baadhi ya watu ambao wanaheshimika, huku baadhi ya waandishi wa habari wakiwa wamekaa kimya, wakiwaangalia wapotoshaji wakichanja mbuga.

Kuna mtu mmoja aliwahi kusema mara nyingi uongo ukiachwa usemwe mara kwa mara unageuka unakuwa ni ukweli na watu wauamini.

Hivi karibuni kumezuka hoja ambazo hazina msingi zikidai eti Simba haijawahi kuingia hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wala fainali ya Kombe la Shirikisho. Kwa bahati mbaya sana kuwa watu wameanza kuamini. Kinachozungumzwa ni kwamba eti wakati wanacheza michuano hiyo ilikuwa haiitwi hivi inavyoitwa sasa.

Ukweli ni kwamba mwaka 1974, Simba iliingia nusu fainali ya Klabu Bingwa Afrika, ambayo kwa sasa ndiyo Ligi ya Mabingwa.

Ilianza kwa kuifunga Linale ya Lesotho jumla ya mabao 9-0, ikishinda ugenini mabao 3-0 na nyumbani 6-0, raundi ya pili ikaitandika Green Buffaloes ya Zambia jumla ya mabao 9-0, suluhu ya ugenini na mabao 9-0 nyumbani, ikatinga hatua ya robo fainali na kuifunga Hearts of Oak ya Ghana, ikitoka suluhu nchini na kwenda kushinda ugenini mabao 2-1, na kutinga hatua ya nusu fainali ambapo mambo hayakuwaendea vema wakatolewa kwa penalti 3-0 na Mehalla el Kubra ya Misri baada ya kila moja kushinda bao 1-0 nyumbani.

Mtu kuibuka leo kusema Simba haijawahi kufika hapo ni uongo mkubwa, kwani kilichobadilika hapo ni jina na mfumo tu, lakini hakuna timu yoyote iliyonyang'anywa taji. Hata Al Ahly iliwahi kutwaa kombe la Afrika wakati ikiitwa Klabu Bingwa Afrika, na mpaka sasa limebadilishwa jina linaitwa Ligi ya Mabingwa hatujawahi kusikia, Shirikisho la Mpira wa Miguu likiipunguzia idadi ya mataji kwa kufuta kile ilichokifanya wakati ikiitwa Klabu Bingwa.

Hata Kombe la Shirikisho Afrika limebadilishwa mara mbili. Lilianza kuitwa Kombe la Washindi barani Afrika, baadaye Kombe la CAF kabla ya 2004 kuitwa Kombe la Shirikisho.

Simba ilifika fainali mwaka 1993 kwa kuitoa Ferroviario de Maputo ya Msumbiji kwa bao la ugenini, suluhu nchini na bao 1-1 ugenini, ikaifunga Manzini Wanderers mabao 2-0, bao 1-0 nyumbani na ugenini, ikaenda kucheza dhidi ya USM El Harrach ya Algeria mabao 3-0, ikishinda mabao 3-0 nyumbani, na kufungwa 2-0 ugenini, ikaifunga Aviacao ya Angola mabao 3-1 nyumbani na kwenda kutoa suluhu ugenini kabla ya kutinga fainali ambapo ilitoa suluhu nyumbani na kufungwa mabao 2-0 nyumbani mgeni rasmi akiwa ni Rais wa awamu ya pili Tanzania, Ali Hassan Mwinyi.

Mfumo au majina kubadilika haiwezi kufuta mataji au rekodi. Huwezi kusema Yanga si mabingwa mara 27 kwa sababu huko nyuma bingwa alikuwa hapatikani kwa kucheza ligi bali ni mfumo wa mtoano kuanzia mechi ya kwanza hadi ya mwisho.

Huwezi kuwanyima Simba ubingwa na Kagame mara sita kwa sababu kabla ya kuitwa Kagame lilikuwa likiitwa Kombe la Afrika Mashariki na watu waanze kuhesabu pale Rais Paul Kagame alipoanza kudhamini.

Yanga haiwezi kupunguziwa ubingwa wake kwa sababu wadhamini wanabadilika mara kwa mara, hivyo kila mdhamini mpya anayeingia ndiyo ianze kuhesabiwa. Wanahabari wanatakiwa wasikae kimya kwa hili. Soka ni mchezo wa rekodi na historia, bila hivyo hakuna soka na ladha yake itapungua.

# Afungwa jela miaka 30 kwa kumbaka kikongwe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Mtaa, Kata ya Chikonji, Manispaa ya Lindi, Saidi Chilemba (49), amehukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani, baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka bibi mwenye umri wa miaka 70 (jina limehifadhiwa).

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Lindi mkoani hapa, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa iwapo anazo sababu za msingi zitakazoishawishi mahakama isimpe adhabu kali kutokana na kosa hilo. Akajitetea asipewe adhabu kali. Ana familia. Anategemewa na wazazi na watoto. Watakosa huduma yake.

Mshtakiwa huyo pia alijitetea kwamba alilazimika kufanya kitendo hicho kutokana na kutekwa na shetani wa mapenzi. Na alifanya kitendo kile bila kujitambua.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batraine alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, iwapo anazo kumbukumbu za makosa ya zamani ya mshtakiwa. Akadai hakuwa na kumbukumbu za makosa, lakini akaiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali, ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya kuwafanya unyama wa aina hiyo dhidi ya wazee.

"Sina kumbukumbu za zamani kwa mshtakiwa, lakini ninaomba mahakama yako tukufu kumpa adhabu kali, kwani kitendo alichokifanya ni udhalilishaji kwa wazee wasio na kosa," alidai Mramba.

Hakimu Batraine, akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 01/2023, alisema hakubaliani na utetezi wa mshtakiwa kupitiwa na shetani. Sheria pia inamfunga mikono. Hivyo, akamhukumu kwenda gerezani kutumikia kifungo cha miaka 30 pamoja na kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. 500,000 amalizapo adhabu yake.

Awali ilidaiwa mahakamani huko na Mwanasheria wa Serikali Mramba kuwa Februari 3, mwaka huu, huko Mtaa wa Chikonji, Manispaa ya Lindi, mlalamikaji (jina linahifadhiwa), akiwa nyumbani kwake amepumzika, mshtakiwa alifika na kumwingilia kwa nguvu bila ridhaa yake.

# Mawaziri watatu waweka msimamo uvamizi hifadhi

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

MAWAZIRI watatu waliotembelea eneo la mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENEPA), wamewataka wananchi kuheshimu sheria na taratibu zilizopo, ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima baina ya wanyamapori na binadamu.

Mawaziri hao ni wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Angellah Kairuki na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, waliotembelea eneo lililowekwa mipaka kwa mujibu wa GN ya mwaka 1968 ya hifadhi.

Katika ziara hiyo, Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alikuwapo kuwapokea mawaziri hao. Walitembelea Kijiji cha Kibaso, Kata ya Kwinhancha wilayani Tarime.

Akizungumza na wananchi hao, Naibu Waziri Masanja alisema ni muhimu wananchi kutambua kila Mtanzania anaishi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Hakuna aliyeko juu ya sheria.

"Nimesikia kuna malalamiko mtu anapokwenda porini (hifadhini) anauawa. Ninawaambia lile pori linatunzwa kwa sheria za nchi na hairuhusiwi shughuli za kibinadamu. Hakuna askari-pori aliyeajiriwa kulinda watu, bali hifadhi na rasilimali zilizomo. Mle mna wanyamapori wakali na waharibifu.

"Anapouawa mwananchi, mnakimbilia kulaumu askari. Ieleweke hawajaariwa kuwalinda nyie. Wanalinda hifadhi na rasilimali zilizomo mle. Mnafuata nini huko? Hii ni kauli ya serikali kwamba mwananchi yeyote haruhusiwi kukanyaga hifadhini. Mle mna wanyama wakali.

"Mbona huendi Jeshi la Magereza? Mbona huendi Jeshi la Wananchi? Mbona huendi polisi kuwachezea?" Ninataka haya malalamiko yakome. Mfuate sheria za nchi. Nani yuko juu ya sheria? Hakuna anayeishi juu ya sheria.

"Mnalalamika lakini acheni kwenda kule. Kuna majangili, majambazi! Huyo askari akulinde wewe, alinde wanyama, majambazi na majangili. Kwanini msifuate sheria, kazi zote hizo (askari) atazifanya? Kwanini usijue sheria za nchi? alihoji.

Naibu Waziri Masanja aliongeza: "Kaeni kwenye maeneo yanayoruhusiwa kisheria, yaacheni mapori na hifadhi zihifadhiwe na wataalamu waliokasimiwa madaraka na serikali. Tumekuja mawaziri hapa tumetumwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Ni ujumbe mahususi wa serikali, mheshimu mapori yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho."

Alisema wanaolalamika kwamba kuna ndugu wameuawa, watambue kuna askari wameuawa, jambo ambalo siyo sawa kwa kuwa wanavamia hifadhi na kutaka waachwe. Halibariki!

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita alisema alikutana na wananchi wa Kitongoji cha Gong'ola ambao eneo zima limechukuliwa na alipeleka hoja kwenye chama, kwa Waziri Mkuu na ndio maana mawaziri wamekwenda eneo hilo.

Waziri wa TAMISEMI, Angellah, alisema "hakuna kipya, wananchi wajue serikali haiwezi kumwibia wala kumdhulumu mwananchi wake. Rais Samia amekuwa mwema, ameacha mita 500 ambazo kwa kawaida zinatakiwa ziachwe kwenye hifadhi lakini wamepewa wananchi.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

TAARIFA KWA UMMA

UANDIKISHAJI WA MAENEO YA KUHIFADHIA BIDHAA

*Dares salaam, Ijumaa, 05 Mei 2023*

**1.0 Utangulizi**

Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuwakumbusha wamiliki (au watumiaji) wa maeneo ya kuhifadhia bidhaa na Umma kwa ujumla kwamba, Sheria ya Fedha, 2022 kifungu cha 45A chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 kinawataka wamiliki (au watumiaji) wa maeneo ya kuhifadhia bidhaa, kusajili maeneo hayo kwa Kamishna Mkuu. Kifungu hicho kilianza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Julai, 2022.

**2.0 Utekelezaji**

Ili kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 45A cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438, wamiliki wa maeneo ya kuhifadhia bidhaa wanakumbushwa kufanya yafuatayo:-

a. Kutoa taarifa za maeneo ya kuhifadhia bidhaa wanayomiliki kwa Kamishna Mkuu kupitia ofisi za TRA, zilizo karibu na eneo la kuhifadhia bidhaa, kwa kujaza fomu maalum Namba ITAX 106.01.E (Fomu ya Usajili wa Maeneo ya Kuhifadhia Bidhaa). Kila eneo la kuhifadhi bidhaa litasajiliwa tofauti hata kama linapatikana ndani ya kiwanja kimoja au nyumba moja.

b. Kujaza ritani ya taarifa sahihi za bidhaa zilizomo kwenye maeneo yao na kuiwasilisha kwa Kamishna Mkuu kila mwezi kwa kutumia fomu Namba ITX 284.01.E. Ritani ya kila eneo lililosajiliwa kwa ajili ya kuhifadhi bidhaa, inapaswa kuwasilishwa kwa Kamishna Mkuu kupitia kwenye ofisi za TRA iliposajiliwa.

c. Kuwasilisha ritani ya taarifa ya bidhaa zilizomo kwenye maeneo yao ya kuhifadhia kila mwezi mnamo au kabla ya tarehe 15 ya mwezi unaofuata mwezi wa ritani hiyo.

d. Endapo itatokea mmiliki/Mtumiaji anaamua kufunga eneo lake, kubadilisha umiliki au kubadili matumizi, atawajibika kuwasilisha taarifa hiyo TRA kupitia Mkoa wa Kikodi husika kwa maandishi.

Mamlaka ya Mapato inaendelea kutoa miongozo na kuelemisha wamiliki (au watumiaji) wa maeneo ya kuhifadhia bidhaa na umma kwa ujumla kuhusu utekelezaji wa matakwa haya ya kisheria. Mamlaka pia inawasihi wamiliki wote wa maeneo ya kuhifadhia bidhaa kujitokeza pale wanapoitwa kwa ajili ya kupewa elimu.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo

| | |
|---|---|
| **Tovuti:** | www.tra.go.tz |
| **Namba ya Bure:** | 0800 750 075 au 0800 780 078 |
| **WhatsApp:** | 0744 23 33 33 |
| **Barua Pepe:** | huduma@tra.go.tz or services@tra.go.tz |

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

**A. J. Kidata**
**Commissioner General**

# Bosi DART aonya unywaji wa pombe kwa watumishi

**Na Joseph Mwendapole**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Edwin Mhede, amesema hatosita kumfukuza kazi mtumishi atakayebainika kwenda kinyume cha maadili ya utumishi wa umma, ukiwamo unywaji wa pombe.

Alitoa hadhari hiyo juzi kwenye ofisi za wakala huo Ubungo, Dar es Salaam alipozungumza na wafanyakazi wa wakala baada ya wafanyakazi hao kupata elimu kuhusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

"Tunahudumia zaidi ya watu 180,000 kwa siku. Sasa huwezi kufanya kazi hii ukiwa umekunywa pombe na hata kanuni za utumishi wa umma zinakataza kabisa kwa mtumishi wake kutumia kilevi.

"Kuna wakati nilikumbusha wafanyakazi wenzangu kwamba tunapaswa kuishi kwa kufuata misingi ya maadili tunapokuwa kazini na hata nje ya kazi na hayo siyo maneno yangu. Ni maelekezo ya serikali.

"Zipo sheria za utumishi wa umma ambazo mimi nimepewa kazi ya kuzisimamia. DART inahitaji nguvu kazi yenye afya inayoeleweka ndiyo maana wote waajiriwa na wale wa mikataba wanapata huduma za afya kwa sababu tunataka watu wenye afya na timamu wahudumie wananchi," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mtumishi akipata fedha ahakikishe anazitumia vizuri na kwa matumizi yake badala ya kuzitumia kufanya vitendo ambavyo vinakwenda kinyume cha maadili ya utumishi wa umma.

Kuhusu kutunza siri, Dk. Mhede alisema watumishi wa umma wanawajibika kwa mujibu wa Kanuni ya 65 (i) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 kutunza siri hasa kuhusu afya ya mtu.

"Suala la kutunza siri ni takwa la kisheria lakini kwenye afya pia suala la kutunza siri linalindwa na sheria. Kwa hiyo, ukisikia mtu amepima na kubainika kuwa na VVU usiende kutangaza. Hayakuhusu!" Alionya.

Alisema amekuwa akikemea mara kwa mara unywaji wa pombe kwa watumishi wa umma na aliwakumbusha kuwa sheria iko wazi kuhusu hatua za kuchukuliwa kwa mtumishi atakayebainika kunywa pombe.

Alisema kuna watumishi wa umma ambao wamekuwa wakishtakiwa na kufukuzwa kazi baada ya kubainika kutumia kilevi. Ni kinyume cha maadili ya utumishi wa umma.

"Tumebeba dhamana ya uhai wa watu na sheria zinataka tuwe walinzi wa watu. Sasa huwezi kulinda watu wakati mwenyewe una tabia za ovyo ovyo. Hatuwezi kuruhusu. Nitakuaminije kukukabidhi uhudumie watu 180,000 kwa siku wakati ni mlevi?" alihoji Dk. Mhede.



Rais wa Chama cha Wachimbaji wa Madini Tanzania (FEMATA), John Bina, akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Kampuni za Nsagali Group, Emmanueli Silanga (kushoto) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mzigwa Mining Investment, Hassan Doyo Hassan, wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa chama cha wachimbaji nchini unaoendelea jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchungaji aona ukakasi shoga kupelekwa gerezani

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MCHUNGAJI wa Kanisa la Moravian Usharika wa Singida Mjini, Yona Mbogo amesema njia pekee ya kupambana na ushoga na usagaji ni kumtegemea Mungu.

Ameonya kuwa kuwakamata na kuwaweka gerezani kwa pamoja wanaojihusisha na vitendo hivyo ni kuongeza ukubwa wa tatizo hilo.

Mch. Mbogo alihadharisha hilo juzi alipohubiri wakati wa ibada ya Jumapili iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Moravian Singida lililopo Mwenge, Manispaa ya Singida.

"Jambo hili la mapenzi ya jinsia moja ni pana. Mfano, unapowakamata wanaojihusisha na vitendo hivyo unakwenda kuwaweka gereza gani? Kwa sababu hivi vitendo vinafanywa kati ya mwanaume na mwanaume, mwanamke dhidi ya mwanamke," alisema.

Mchungaji huyo alisema kuwa kutokana na mazingira ya jambo hilo yalivyo, njia pekee inayoweza kusaidia kukabiliana na vitendo hivyo ni jamii kuendelea kuzingatia masuala ya maadili kuanzia ngazi za familia na kuwa na matumaini kwa Mungu ili aiepushe jamii na janga hilo.

Alisema kuporomoka kwa uchumi wa kipato kwa jamii ndiko kumetoa mwanya kwa baadhi ya wafadhili kupenyeza fedha kupitia taasisi zisizo za kiserikali (NGO) na watu binafsi ambao wamekuwa wakizitumia kuhamasisha vitendo hivyo.

Akizungumzia suala la utoaji wa sadaka na zaka, mchungaji huyo alisema ni jambo kubwa katika imani kwa kuwa mtu anayemtolea Mungu zaka kwa ukamilifu, imwongezea maradufu tofauti na yule anayekuwa mwizi wa kumwibia zaka hiyo.

Alisema Mungu amehimiza kutolewa zaka asilimia 10 kutoka mapato ya kila kitu kinachopatikana iwe mshahara, mazao, mifugo na vinginevyo.

Alisema mtu anapotoa zaka kwa uaminifu, Mungu anatengeneza agano kati yake pamoja na kizazi chake chote. Alimtolea mfano Abrahamu jinsi alivyobarikiwa baada ya kutoa kwa unyenyekevu na uaminifu. Akawa tajiri mkubwa.

Mchungaji Mbogo alisema kutoa zaka kwa Mungu isiyo kamili inaleta laana kwa vizazi hadi vizazi na kusababisha mtu kupata matokeo mabaya ya maisha yake, ikiwamo mikosi kama kufukuzwa kazi, kufeli masomo, magonjwa, biashara kudorora, kupata fedha lakini zinapotea pasipo sababu kutokana na matumizi yasiyofahamika na mengine mengi yanayofanana na hayo hadi kufikia hatua ya kudhani amerogwa.

Alisema mtu akishindwa kutoa sadaka ya Sh. 500 hata akipata Sh. milioni moja hatoweza kutoa, hivyo aliwaomba waumini wa kanisa hilo kujenga tabia ya kumtolea Mungu sadaka na zaka na Mungu atawabariki na vizazi vyao.

Mch. Mbogo, akizungumzia umuhimu wa kwenda kusali, alisema kuna watu wamekuwa wakichelewa kwenda ibadani kwa kutoa visingizio mbalimbali vikiwamo kukosa nauli au mtoto ni mgonjwa lakini watu haohao wanapokuwa na jambo lao la kupata fedha, wako tayari kukodi bodaboda ili wafike kwa wakati.

"Jambo hili sio zuri na halimpendezi Mwenyezi Mungu. Ninawaombeni wakristo kujenga tabia ya kuwahi kufika kanisani mapema. Tuacheni tabia ya kuwa na sababu mbalimbali," alisema.

Katika ibada hiyo Mch. Mbogo aliwaombea maombi wanafunzi wa Sekondari ya Mwenge ambao wanafanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita.

# Wafa kwa kufukiwa na kifusi cha mgodi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WATU wawili wamefariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi katika mgodi wa dhahabu eneo la Bingwa, Kijiji cha Rwamgasa mkoani Geita.

Waliyofariki dunia ni Eliasi Josefu (25), mkazi wa Mkoa wa Singida na Wiliam Mhamedi (30), mkazi wa Nyankumbu, Wilaya ya Geita.

Akizungumza eneo la tukio, Mwenyekiti wa Kijiji cha Rwamgasa, Musa Songoma alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Mei 6 mwaka huu katika eneo hio la Bingwa.

Songoma alisema eneo hilo lilikuwa linasimamiwa na Mwananyanzala na lilikuwa limefungwa na mashimo yote yalikuwa yamefukiwa, lakini wawili hao waliingia kwa siri kuchimba dhahabu ndipo wakafukiwa na kifusi na kufariki dunia.

Alisema miili yote ya wachimbaji hao ilitolewa kwenye shimo na wananchi wa kijiji hicho na baada ya kutolewa walichukua miili yote miwili na kuipeleka katika chumba cha kuhifadhi maiti katika Kituo cha Afya Katoro.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Rwamgasa, Emmanuel Alphoce, aliwataka wachimbaji wafuate utaratibu na wakishazuiwa kuingia eneo husika, wanatakiwa wasikie.

"Shida ni kwamba watu hao walikuwa wanakwenda kuiba, wanaingia kuchimba kwenye ardhi ambayo kipindi hiki kuna mvua kubwa inaendelea kunyesha. Kwa hiyo, ardhi imeshakuwa laini, na bahati mbaya mtu akiwa anakwenda kuiba haangalii usalama wake," alisema.

"Ndiyo maana mimi ninasema wachimbaji wanatakiwa kufuata utaratibu na maelekezo ya viongozi wao. Viongozi waliona kwamba sehemu hii haitakiwi kuchimbwa na wakaizuia na kuweka ulinzi, watu walipoona kuna ulinzi wakaacha kuchimba pale.

"Walinzi baada ya kuona watu hawafiki pale, waliondoka pale na kurudi kwenye eneo lao la kazi ndipo watu wakapata mwanya wa kwenda kuchimba kwa wizi," alieleza zaidi Ofisa Mtendaji huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Safia Jongo, alipoulizwa na Nipashe kuhusiana na tukio hilo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa wanaendelea na uchunguzi zaidi.



# Kusuasua miradi ujenzi barabara kwamkera RC

**Na Mary Mosha,** HAI

KUSUASUA kukamilika kwa wakati kwa miradi ya ujenzi wa barabara za kiwango cha lami, zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), katika Wilaya ya Hai, kumemkera Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu na kuagiza makandarasi waliopewa miradi hiyo, kuheshimu makubaliano ya mkataba.

Babu, aliwaonya makandarasi hao mwishoni mwa wiki, wakati alipokwenda kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara za Bomangombe/Kikavuchini yenye urefu wa kilomita 0.5, ambayo inajengwa kwa gharama ya Sh. milioni 299 na barabara ya TTCL/RC Church.

Barabara nyingine alizokagua ni ile ya St. Dorcas/Polisi/Relini, Kituo cha Mabasi Hai/Kingereka/Nyerere Road kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 1.805 ambayo inagharimu zaidi ya Sh. milioni 952.595.

"Ninyi makandarasi mliopewa kazi hii, mnapopewa miradi ya barabara, tekelezeni kwa wakati na kwa ubora ili msiingie katika mgogoro na serikali; lakini pia lengo ni kuwarahisishia wananchi kusafirisha mazao yao kupitia barabara hizi. Nitakuwa mkali kwa wale watakaoshindwa kuheshimu makubaliano ya mkataba," alisema.

Akitoa taarifa kuhusu miradi hiyo, Meneja wa TARURA wa Wilaya Hai, Kuya Francis, alisema barabara hizo nne zilikumbwa na matatizo ya kutokamilika kwa wakati, kutokana na uhaba wa maji kwa ajili ya matengenezo ya barabara wakati wa kiangazi.

"Kimsingi hali hiyo iliathiri shughuli za ujenzi na kusababisha makandarasi kuwasilisha ombi la kuomba nyongeza ya muda ili kukamilisha kazi zilizo baki. Hata hivyo, barabara hizi zimefikia asilimia 70 ya ujenzi."

Akiwa Wilaya ya Hai, mwaka jana alipotembelea miradi hiyo, Mtendaji Mkuu wa TARURA nchini, Victor Seff, alisema hataki kuona mradi hata mmoja wa ujenzi wa barabara za vijijini au mjini, unakwama kutokana na mkandarasi kuja na kisingizio cha kutolipwa fedha zake au kukosa malighafi.

Alisema anataka kusikia kila wilaya na kila mkoa, mkandarasi amemaliza mradi kabla ya wakati na hana madai ya fedha au wahandisi kufanya ucheleweshaji wa malipo.

# Tishio umwagaji damu lamshtua Mkuu wa Wilaya

**Na Tumaini Mafie,** MONDULI

TISHIO la umwagaji damu lililotolewa na familia mbili za kifugaji katika Kijiji cha Lendikinya, Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, limemshtua Mkuu wa Wilaya hiyo, Joshua Nassari.

Amesema kutokana na tishio hilo, amelazimika kuingilia kati kutafuta amani baina ya pande mbili zinazozozana kuhusu uhalali wa umiliki wa ardhi.

Anayedaiwa kumiliki ardhi hiyo yenye ukubwa wa ekari 26 kwa mujibu wa sheria za ardhi ni Nakudana Mungaya, lakini familia mbili za kifugaji zinazowahusisha, Yamat Mbaranot na Mbarnot Marmalu, zinadai ardhi hiyo ni mali yao na wanaimiliki kihalali. Akizungumzia mgogoro huo mwishoni mwa wiki, Nassari, alisema amelazimika kuingilia kati mgogoro huo kutokana na kutishia amani ya wakazi Lendikinya pamoja na kuhatarisha maisha ya familia zinazogombana.

"Walikuwa na kesi katika Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya na iliamuliwa kwa Nakudana Mungaya kupewa haki ya umiliki wa ardhi hiyo. Sasa baada ya uamuzi huo kutolewa, walalamikiwa Yamat Mbaranot na Mbarnot Marmalu, hawakuridhika na uamuzi uliompa haki Nakudana.

"Kutokana na kutokubaliana na uamuzi huo wa baraza, Yamat Mbaranot na Mbarnot Marmalu, waliendelea na msimamo wao wa kugomea kuachia ardhi hiyo na kutishia kumwaga damu. Ndiyo maana nikaenda eneo husika lenye mgogoro na kuagiza wote wafike ofisini kwangu tulimalize hili sakata kwa amani."

Nakudana, alipewa ushindi katika shauri namba 125 la mwaka 2007 lililoamliwa na baraza hilo. Alipata ushindi huo uliotolewa na Mwenyekiti wa baraza hilo, Fadhili Mdachi, aliyeamuru eneo lenye shamba lenye mgogoro lenye ukubwa wa ekari 26 lililopo Moranda katika kijiji hicho kuwa ni mali ya mlalamikaji.

Kabla ya Nassari kuingilia kati mgogoro huo, Nakudana, alilalamika akidai kutishiwa maisha na wanakijiji wenzake walioungana na walalamikiwa katika mgogoro huo.

Kutokana na mgogoro huo, Nakudana, amemwomba Mkuu wa Wilaya ya Monduli, kuipa ushirikiano kampuni ya udalali ya Regiz Co. Ltd ya Jiji la Arusha kutekeleza amri halali ya baraza hilo ya kuwaondoa kwenye ardhi yake walalamikiwa walioshindwa kesi hiyo.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Baraka Kanunga, akizungumza kwenye kikao cha wadau wa ufugaji kuhusu biashara ya mifugo kwenye minada, mji mdogo wa Orkesumet juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanaojitolea misaada kibinadamu wapongezwa

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

UHITAJI mkubwa wa misaada ya kibinadamu kuwafariji yatima wanaolelewa na kutunzwa katika Kituo cha Light in Afrika kilichoko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, umewagusa wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuamua kukipiga jeki.

Pia wakazi hao wa Kanda ya Ziwa wanaounda kikundi cha Nyanza Group katika eneo hilo, limewakumbuka pia wagonjwa waliolazwa Kituo cha Afya Mirerani, kwa kukipatia vifaa mbalimbali.

Mwenyekiti wa Nyanza Group (Mirerani), Malimi Kija, akizungumza na Nipashe jana, alisema mioyo ya hisani na kujitolea ya wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa imewasukuma kusaidia kituo cha afya na watoto hao.


Alisema kikundi chao chenye wanachama 100 kinaiunga mkono serikali kwa kujitoa kupitia mifuko yao kwenye vikwazo vya kijamii ili wahitaji hao wajisikie kama binadamu wa kawaida.

"Tumeguswa kutoa kidogo tulichokipata na kuwapa wahitaji ili nao wapate faraja kama Watanzania wengine. Kikundi chetu kinapenda jamii inayotuzunguka inufaike na kile tunachojaliwa na Mwenyenzi Mungu katika shughuli zetu hapa Mirerani. Sisi kaulimbiu yetu Nyanza Group ni kuwezeshana na kufikia jamii katika mahitaji," alisisitiza.

Awali, Katibu wa Nyanza Group, Daniel Ndaikya, alisema misaada inayotolewa kwenye Kituo cha Afya Mirerani na Kituo cha Watoto Yatima cha Light in Africa, ina thamani ya Sh. milioni 1.5.

Kwa mujibu wa Ndaikya, fedha hizo zimetokana na michango binafsi ya mtu mmoja mmoja kupitia Nyanza Group ili kusaidia jamii inayowazunguka kwenye mji huo wa Mirerani.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya mji mdogo wa Mirerani (TEO), Isack Mgaya, aliwapongeza wanachama na viongozi wa kikundi hicho kwa kujitolea misaada hiyo.



# HABARI KANDA YA ZIWA

## RC ahimiza uchimbaji madini rafiki kwa mazingira

**Na Mohab Dominick,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, amelitaka Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Tanzania (FEMATA), kusimamia suala la utunzaji wa mazingira kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini ili wasiwe sehemu ya uharibifu wa mazingira kutokana na asilimia kubwa ya wachimbaji hao kunyooshewa kidole uharibifu wa mazingira.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa akifungua maonesho wiki ya madini, kongamano la wachimbaji na mkutano mkuu wa FEMATA yanayoendelea kitaifa jijini hapo

Alisema Mwanza wana upandaji wa miti milioni 20 huku akitaja kampuni moja iliyojitolea miti milioni tatu lengo likiwa ni kuhakikisha Tanzania inakuwa ya kijani.

"Kwenye utunzaji wa mazingira bado hili linanisumbua inaonesha wachimbaji ni watu wasiojali, niwatake kutekeleza shughuli zenu kwa kutunza mazingira," alisema Malima.

Maonesho hayo yaliyofunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza yanatarajiwa kuhitimishwa Mei 10 na kufungwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa huku uongozi wa FEMATA ukitakiwa kueneza elimu ya utunzaji mazingira kwa lengo la kudhibiti hali ya jangwa nchini.

# Jafo awajia juu wafugaji uharibifu vyanzo vya maji

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amepiga marufuku wafugaji kuingiza na kunywesha mifugo yao katika mabwawa ya maji hali inayosababisha kuchafua kwa kujaza tope na upotevu wa vyanzo hivyo.

Alitoa kauli hiyo juzi katika mradi wa bwawa la maji katika Kijiji cha Kiloleli baada ya ziara yake wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, kukagua na kuweka jiwe la msingi na kuzindua baadhi ya miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi ambayo inatekelezwa katika wilaya hiyo.

"Taarifa niliyopokea ni kwamba bwawa hili limefanyiwa marekebisho kutokana na kujaa tope na kupunguza kina cha maji hali inayotishia kutoweka kwake, lakini sasa hivi limetengenezwa na kutolewa tope lote ni marufuku sasa kuingiza mifugo kunywa maji ndani ya mabwawa ya maji tumieni mabirika ambayo yatajengwa," alisema Jafo. Aliwataka pia wananchi wa wilaya hiyo kuacha kufanya shughuli za kilimo katika mabwawa ya maji ambayo yamejengwa kandokando ya vyanzo vingine vya maji kwa kuvitunza pamoja na kupanda miti kwa wingi ili viendelee kuwahudumia wakati wote.

Katika hatua nyingine Waziri Jafo, aliziagiza halmashauri zote nchini kutekeleza agizo la upandaji miti milioni 1.5 kwa kila mwaka, pamoja na kuhamasisha kampeni ya soma na mti ambayo inataka kila mwanafunzi kupanda mti ili kuendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, alisema walipokea Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi, ambayo inatekelezwa katika kata mbili ya Lagana na Kiloleli, na kueleza kuwa imekuwa na tija kwa wananchi katika utunzaji wa mazingira.

Alisema miradi hiyo ni unenepeshaji mifugo ambao uliwekewa jiwe la msingi na Waziri Jafo, mabwawa ya maji na kiwanda cha kuchakata bidhaa za ngozi ambao aliuzindua.

Alitaja miradi mingine inayotekelezwa wilayani Kishapu kwa lengo la kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kuwa ni ujenzi wa majosho ya kuoshea mifugo, utengenezaji wa majiko banifu yatakayosaidia kupunguza matumizi ya kuni na kuacha kukata miti ovyo, ufugaji nyuki, kilimo cha zao la mkonge na upandaji miti.

Baadhi ya wananchi ambao ni wanufaika wa miradi hiyo, waliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi hiyo katika maeneo yao ambao licha ya kutunza mazingira, pia imekuwa ikiwasaidia kuwaingizia kipato na kuendesha maisha yao.




Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa hundi ya dola 10,000 kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya watoto wenye mahitaji maalum ya Buhangija iliyoko Manispaa ya Shinyanga, Fatuma Gilalah (wa nne kulia) na Ofisa Elimu ya Msingi (wa pili kushoto). Msaada huo umetokana na sehemu ya fedha zilizotolewa na Taasisi ya Nos Vies en Partage (NVeP), inayofadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Barrick Gold Corporation, Mark Bristow. Hafla ya kukabidhi msaada huo ilifanyika katika mgodi wa Bulyanhulu mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zahanati yatelekezwa kwa kukosa watumishi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAHANATI mpya yenye thamani ya Sh. milioni 170 iliyojengwa kwa nguvu za wananchi na wachimbaji wadogo wa Mgodi wa Nyamishiga, Kata ya Lunguya Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga imetelekezwa baada ya kukamilika kutokana na kukosa wahudumu wa afya.

Zahanati hiyo ambayo imejengwa kwa lengo la kusogeza huduma za afya karibu na wachimbaji hao pamoja na wananchi wanaowazunguka, kuondoa gharama za kusafirisha wagonjwa hadi katika Kituo cha Afya Bugarama, bado haijafunguliwa hadi sasa licha ya kukamilika.

Hayo yalibainishwa na Diwani wa Kata ya Lunguya, Benedictor Manwari, katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2022/2023 wakati akichangia taarifa ya utekelezaji wa kamati ya elimu, afya na maji kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Machi kuwa serikali inatakiwa kuwaunga mkono wawekezaji wadogo katika miradi wanayoitekeleza kwa maendeleo ya jamii.

Aidha alisema, wachimbaji wa Nyamishiga wamefanikiwa kujenga zahanati hiyo, lakini imeshindwa kufunguliwa na kutoa huduma kwa ukosefu wa watumishi huku wakiahidi kununua gari la wagonjwa endapo itafunguliwa na kuanza kutoa huduma mapema.

"Zahanati hii imekamilika na kilichobaki ni kufunguliwa na kuanza kutoa huduma, kuna majengo yote na vitu vya muhimu kwa ajili ya kutoa huduma na hivi karibuni wameleta tofali 3,000 kwa ajili ya kujenga nyumba ya watumishi hivyo tuwaunge mkono kwa kuanza kutoa huduma," alisisitiza Manwari.

Diwani Mwakata Ibrahimu Masanja, alisema kuna majengo ya zahanati 20 yamekamilika na yamejengwa kwa nguvu za wananchi na yanahitaji watumishi, bora wakaazima watumishi kutoka vituo vya afya vinavyofanyakazi na kuanza kutoa huduma.

Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Flora Sagasaga, alisema, zahanati zimekamilika baadhi zimejengwa kwa nguvu za wananchi na nyingine kupitia fedha za mapato ya ndani zinazotokana na wadau wa maendeleo (CSR), wataazima watumishi na kwenda kuwahudumia wananchi huku wakisubiri serikali kuajiri watoa huduma kwa kipindi hiki.

Aidha, alimtaka Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Charles Fussi, kujenga vyoo katika minada na magulio ambayo yanaingizia mapato halmashauri na minada hiyo hususan ya Bulige na Masabi kwa kuwa wachuuzi wake wanajisaidia vichakani na kuhatarisha usalama wa afya kwa wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo.

Nipashe Spotika



SABABU 4 POCHETTINO KUFITI UKOCHA CHELSEA UK. 12-13




ERIC MAXIM CHOUPO

# KLABU 3 ZA ULAYA AMBAZO HAZIJAPOTEZA NYUMBANI

**BARCELONA,** Hispania

MSIMU wa 2022-23 unapokaribia mwisho wake, klabu kadhaa za soka kote Ulaya zinawania nafasi za juu katika ligi zao. Ingawa timu nyingi zina rekodi za kuvutia nyumbani, ni chache tu zilizochaguliwa zimeweza kucheza msimu nzima wa ligi bila kupoteza mchezo wowote wa nyumbani.

Katika makala haya, tutaangalia kwa karibu klabu tatu ambazo ziko mbioni kufikia mafanikio haya ya kuvutia katika ligi tano bora za Ulaya. Tutachunguza mikakati yao, wachezaji wakuu, na kuchanganua jinsi walivyoweza kudumisha rekodi ya nyumbani.

Hivyo wacha tuzame na kuona klabu tatu ambazo hazijapoteza michezo ya ligi ya nyumbani msimu wote.

NB: Zingatia hii ni kabla ya mechi za mwishoni mwa wiki.

**#3 Union Berlin**

Union Berlin wanafanya vyema katika Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu huu. Tangu kupanda Ligi Kuu katika msimu wa 2019-2020, kupanda kwao kumekuwa kwa kasi na kuvutia. Walimaliza katika nafasi ya 11 katika msimu wao wa kwanza katika Ligi Kuu ya Ujerumani, ikifuatiwa na kumaliza kwa kuvutia katika nafasi ya saba na ya tano katika misimu iliyofuata.

Msimu huu, wamekuwa wa kuvutia tu. Sio tu kwa sababu wameshangaza kila mtu kwa kuwa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini kwa sababu hawajapoteza nyumbani kwenye ligi msimu mzima. Klabu hiyo imecheza jumla ya mechi 14 za nyumbani kwa sasa, ikishinda tisa kati ya hizo na sare tano. Katika harakati hizo, wamefunga mabao 25 na kuruhusu tisa pekee.

Union Berlin wanacheza mfumo wa 3-5-2 msimu huu wakiwa na msisitizo mkubwa katika kulinda. Wamekuwa bora katika kukamata timu wakati wa mapumziko na kuzindua mashambulizi ya kukabiliana. Kuhusiana na hili, Sheraldo Becker, Janik Haberer, na Robin Knoche wamekuwa wachezaji muhimu katika uendeshaji wa timu, wakitoa mchango mkubwa zaidi wa mabao katika safu ya ushambuliaji, kiungo na ulinzi kwa pamoja.

**#2 Bayern Munich**

Ingawa Bayern wanaweza kutokuwa na misimu bora kabisa, mabingwa hao watetezi wa Bundesliga bado hawajafungwa nyumbani kwenye ligi msimu huu. Tangu kumteua Thomas Tuchel kama kocha wao, wametatizika kupata kiwango bora. Walistahimili matokeo mabaya ambayo yaliwafanya wasambaratike kutoka kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na DFB-Pokal na kupoteza nafasi yao ya kwanza kwa Borussia Dortmund kwenye msimamo.

Klabu hyo ya Bavaria kwa ujumla inajulikana kwa mfumo wake wa 4-2-3-1, ambao unasisitiza kumiliki mpira huku wakiwakandamiza wapinzani wao. Katika mechi 14 za ligi ya nyumbani msimu huu, wameshinda mechi tisa na kutoka sare tano. Hata hivyo, wamefunga mabao 44 na kufungwa 14 wakiwa nyumbani.

Kwa upande wa wachezaji muhimu katika mbio hizi, Jamal Musiala anajitokeza kwa kuwa ana mchango mkubwa wa mabao ndani ya timu - mabao 15 na asisti 13 katika mashindano yote. Mabao 17 ya Eric Maxim Choupo-Moting yamekuwa muhimu pamoja na uwezo wa Alphonso Davies kuunganisha safu ya ulinzi na mashambulizi kwenye nafasi yake ya beki wa kushoto.

**#1 Barcelona**

Barcelona wamekuwa katikati ya takwimu za kuvutia msimu huu na wako mbioni kuvunja rekodi chache. Kutokana na uchezaji wao mzuri wa ulinzi, timu hiyo haijapoteza mchezo wowote wa nyumbani wa Lgi Kuu Hispania, LaLiga. Wamecheza mechi 15 kati ya hizo, wakishinda 12 na kutoka sare tatu.

Kinachoshangaza zaidi ni ukweli kwamba wameruhusu mabao mawili pekee nyumbani kwenye La Liga msimu huu, wakionesha kiwango chao cha kipekee katika safu ya ulinzi. Kama ilivyozoeleka chini ya uongozi wa Xavi, timu hucheza mpira wa kumiliki katika mfumo wa 4-3-3. Barcelona wanafanikiwa kuwatawala wapinzani wao kwa kushika mpira na kushambulia bila kuchoka.

Kwa kadiri wachezaji wakuu wanavyoenda, mabao 28 ya Robert Lewandowski katika mashindano yote yamekuwa moja ya neema za kuokoa za Barca msimu huu. Hata hivyo, timu hiyo imekuwa na wakati mgumu wanapokosekana Frenkie de Jong na Pedri, ambao bila shaka ni wachezaji wao waliofanya vizuri zaidi. Kwenye safu ya ulinzi, Ronald Araujo amekuwa akivutia sana.

## ISIKUPITE

WAMILIKI wa Klabu ya Manchester City inayoshiriki Ligi Kuu ya England, wanasema wanataka kusaidia soka la Brazil kukua kiuchumi baada ya kundi hilo kununua klabu yake ya 13 ya Bahia. Bahia ambayo jina lake kamili ni Esporte Clube Bahia ndio klabu ya hivi punde zaidi kujiunga na Kundi la Soka la City Football Group (CFG). Klabu hiyo inashiriki ligi kuu ya kitaifa ya Brazil na imeshinda taji hilo mara mbili, mara ya mwisho ikiwa ni mwaka 1988. City Football Group, yenye makao yake makuu Uingereza; hisa nyingi zikimilikiwa na Abu Dhabi United Group inayoongozwa na Sheikh Mansour.



# SABABU NNE POCHETTINO KUFITI UKOCHA CHELSEA FC



**LONDON,** England

CHELSEA imeripotiwa kukaribia kumwajiri Mauricio Pochettino kama kocha wao mpya baada ya The Blues hao kuamua kumfukuza Graham Potter mwanzoni mwa Aprili. Umepita takribani mwaka mmoja tangu Todd Boehly & Clearlake Capital wachukue mikoba ya umiliki hapo Stamford Bridge, lakini haijapita miezi 12 ya kupendeza.

**Wamiliki hao walimfukuza Thomas Tuchel Septemba na kumwajiri Potter, na kumwachia aende miezi saba baadaye.**

Frank Lampard ameajiriwa kama kocha wa muda, lakini klabu hiyo inahitaji mwelekeo mpya baada ya matumizi makubwa msimu huu. Kwa hiyo, kuajiriwa kwa Pochettino kunaweza kuwa uteuzi mzuri kwa Chelsea, haswa baada ya Julian Nagelsmann na Luis Enrique kuripotiwa kuwa nje ya kinyang'anyiro hicho.

Kwa maelezo hayo, hebu tuangalie sababu nne kwa nini Pochettino atafaa kuwa kocha pale Chelsea.

### #4 Kukuza wachezaji wachanga

Tottenham Hotspur watakuwa na kumbukumbu nzuri za Pochettino na moja ya sababu kuu nyuma yake ni uwezo wake wa kukuza wachezaji wachanga.

Wachezaji watatu Dele Alli, Heung Min-Son na Harry Kane walistawi chini ya Muargentina huyo. Kieran Trippier pia aligeuzwa kuwa beki wa kulia wa kiwango cha kimataifa na kuchukua nafasi ya Kyle Walker. Kwa hiyo, hakika anajua njia ya kuwazunguka wachezaji wachanga, ambayo inaweza kuwa sababu kubwa nyuma ya Chelsea kumteua.

The Blues hao wametumia fedha nyingi katika kipindi cha miezi 10 iliyopita, huku wachezaji 15 wakiongezwa kwenye kikosi na 11 kati yao wakiwa chini ya umri wa miaka 25. Mason Mount, Kai Havertz, Christian Pulisic, Armando Broja, Lewis Hall, Reece James, Conor. Gallagher, na Trevoh Chalobah pia wanaangukia katika mabano hayo ya umri.

Isitoshe, chipukizi Levi Colwill na Ian Maatsen, ni miongoni mwa wachezaji wengine waliotolewa kwa mkopo, wamevutia na wana uwezekano wa kutaka kupigania nafasi kwenye kikosi msimu ujao.

Kwa hiyo, kuna vipaji vingi vya vijana vya kuboresha na kukuza, licha ya ukweli kwamba kutakuwa na mauzo makubwa pia msimu huu wa joto. Pochettino inasemekana anataka The Blues kuangazia zaidi vipaji vya nyumbani, na hii ni ishara nzuri kwa klabu ambayo inataka kujenga kikosi cha vijana na wenye njaa ya kushinda mataji.

Uteuzi wake unaweza pia kumshawishi Mason Mount kusaini mkataba mpya, huku Pochettino akiripotiwa kuwa shabiki wa mchezaji huyo.

### #3 Kuunda kikosi cha mafanikio

Ingawa Pochettino hakufurahia mafanikio makubwa katika klabu ya Paris Saint-Germain (PSG), muda wake akiwa Tottenham Hotspur ulikuwa wa maana zaidi kwani alifuzu kwa kuwachomoa wachezaji bora zaidi kati ya waliokuwa na kiwango cha chini.

Wachezaji kama Moussa Dembele, Ben Davies, Harry Winks, Moussa Sissoko, na wengine wengi waliimarika sana wakati wa utawala wa Pochettino klabuni hapo.

Chelsea, kama Tottenham mwaka 2014, wana kikosi kichanga na nyota wenye uzoefu. Hata hivyo, ni kikosi ambacho hakina mafanikio makubwa, kutokana na vipaji vyao na uwezo wao na uchezaji katika klabu zao za awali.

Wachezaji kama Kai Havertz, Kalidou Koulibaly, Mykhailo Mudryk, Marc Cucurella, Hakim Ziyech, na Christian Pulisic wamekuwa chini ya viwango kwa muda wa miezi 12-18 iliyopita.

Lakini Pochettino bila shaka anaweza kubadilisha nguvu hii kwa kuunda mifumo unaowaruhusu kustawi.

Pia kuna suala la Romelu Lukaku, ambaye amekuwa na kipindi kizuri cha pili cha msimu akiwa kwa mkopo Inter Milan. Mbelgiji huyo alisajiliwa kwa ada ya rekodi ya klabu wakati huo ya pauni milioni 97.5 lakini alitolewa kwa mkopo msimu wa joto kufuatia msimu mbaya ndani na nje ya uwanja.

Bado haijafahamika kama ana mustakabali ndani ya Chelsea, lakini kumtumia ipasavyo kunaweza kumpa Pochettino namba 9, kitu ambacho klabu hiyo inakihitaji sana.

Msimu wa sasa umeonyesha ukosefu wa matumizi sahihi ya vipaji katika klabu. Kwa hivyo, Pochettino anaweza kufanya moja ya malengo yake kuu ni kubadilisha hali ya wachezaji kama hao na kuwasaidia kutambua uwezo wao haraka iwezekanavyo.

### #2 Uzoefu mkubwa wa Ligi Kuu

Kazi ya mwisho ya usimamizi ya Pochettino inaweza kuwa Ufaransa, lakini sio siri kwamba moja ya nyakati zake nzuri zaidi kwenye ukocha ilikuwa miaka mitano pale London Kaskazini.

Tottenham ilimwajiri msimu wa joto wa 2014 baada ya mwaka mzuri sana kule Southampton. Katika misimu yake mitano, aliisaidia klabu hiyo kumaliza katika nafasi nne za juu mara nne. Klabu hiyo ilimaliza katika nafasi nne za juu mara mbili tu ndani ya miaka 22 kabla ya kuteuliwa kwake. Kwa hiyo, hakika aliifanya Spurs kuwa na nguvu.

Kwa hiyo, Pochettino hakika anajua jinsi ya kuunda timu ambayo inaweza kushiriki kikamilifu katika Ligi Kuu, jambo ambalo limekuwa baya pale Stamford Bridge msimu huu. The Blues hao hawajashinda taji la ligi tangu mwaka 2017 na tangu wakati huo pia hawajawa kuwa katika mbio za kuwania, huku Manchester City na Liverpool zikitawala.

Maurizio Sarri, Frank Lampard, na Thomas Tuchel walijaribu kubadilisha simulizi hiyo, lakini walishindwa au hawakuweza kudumisha changamoto ya ubingwa kwa zaidi ya miezi sita.

Timu za Pochettino ni endelevu zaidi, ingawa hakuzungusha kikosi chake vya kutosha pale Tottenham. Lakini Chelsea hakika wana kikosi chenye kina na chenye uwezo wa kufanya kazi nacho na kocha huyo wa Amerika Kusini anaweza kuwasaidia kuwa thabiti zaidi kwenye ligi. Kurejea kwenye nafasi nne za juu itakuwa moja ya vipaumbele vyake.

### #1 Mbinu katika michezo mikubwa

Pochettino, wakati wa Espanyol, Southampton, Tottenham, na PSG, hakuwahi kutawala mechi dhidi ya timu yoyote kubwa.

Hata hivyo, ni vyema kutambua kwamba, ukiondoa PSG, hakuna timu yake iliyowahi kushinda mataji au kuwa na timu ya viongozi. Lakini Pochettino alikuwa na njia yake ya kuzichambua timu zake na moja ya ishara za kwanza za ustadi wake wa kimbinu ilikuwa ushindi wa Espanyol wa 2-1 ugenini dhidi ya Barcelona ya Pep Guardiola mnamo 2009.

Ingawa hakuweza kamwe kuangusha timu yoyote ya juu akiwa na Southampton, maonesho yalikuwa ya kutia moyo. Hata hivyo, wakati alipokuwa Tottenham, rekodi ya Pochettino iliboreka kidogo, kama inavyopaswa kuwa.

Wakati wa kukutana mara 10 na Arsenal kama kocha wa Spurs, walishinda mara nne na kuandikisha sare mbili. Alikuwa na rekodi sawa dhidi ya Chelsea na pia aliandikisha ushindi mara nne katika mechi 10 dhidi ya Manchester United. Ingawa kiwango cha timu yake dhidi ya Liverpool na Man City hakikuwa kizuri sana, alimshinda Guardiola kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi mbili za msimu wa 2018/19.

Lakini mbinu za Pochettino ni nzuri na zenye nidhamu ya ajabu. Ana ubora wa kuongeza mabeki wake wa pembeni na kuipa ulinzi uhuru kidogo. Vile vile, anaweza kufundisha uchezaji wa ushambuliaji thabiti na mzuri ilhali safu yake ya kati inaweza kuwa mbunifu na pia kufanya kazi kwa uharaka.

Ni mtu anayeongozwa na kanuni badala ya mifumo na anaweza kuzoea kikosi badala ya kununua wachezaji wanaoendana na aina yake ya uchezaji. Hiki ndicho ambacho Chelsea wanakihitaji kwa sasa kwani kuongeza fedha nyingi msimu wa joto tena haiwezekani.

## Nukuu

"Baadhi ya wachezaji wachanga ambao wameingia kwenye klabu labda hawajapata nafasi ya kutulia, kujisikia vizuri ndani ya timu, kuelewa mabeki wa pembeni watapishana nao vipi, au wachezaji wa kiungo wanaowaunga mkono. Huo ni mchakato, na unahitaji kazi. Labda ni kazi ambayo sijaweza kufanya katika jukumu hili kama la muda," **Kocha wa muda wa Chelsea Frank Lampard akielezea wachezaji wa kikosi chake.**



"Hisia zangu nyakati fulani hubadilika. Lakini mwisho ni mali ya wachezaji, wanatakiwa kujiridhisha wenyewe na timu na si kwa sababu nasema kitu. Lazima wapate imani yangu. Wote, sio Kalvin tu, wote ni jinsi wanavyofanya. Timu zinabadilika sana na wachezaji wa misimu iliyopita ambao walikuwa muhimu sana lakini msimu huu sio muhimu sana. Ni jinsi wanavyofanya, mambo mengi yanaweza kutokea," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola akizungumzia kuhusu majaliwa ya Kalvin Phillips kuwa yapo mikononi mwake.**



"Tunataka kuweka kipaji chetu bora, hasa wachezaji ambao wanastahili kutambuliwa. Nadhani amekuwa wa ajabu tangu aliporejea kutoka kwa kipindi chake cha mkopo na tunataka kumzawadia, hilo ni la uhakika. Tutapata wakati muafaka wa kufanya hivyo. Ni wazi mkurugenzi wa ufundi Edu na bodi wako juu ya kila mazungumzo kuhusu mkataba mpya na sasa tunafanya kila tuwezalo kufanya hivyo kwa wakati ufaao," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akizungumza kuhusu mazungumzo ya mkataba mpya wa mlinzi wake, William Saliba.**



Nipashe
# Spotika



CHELSEA imeripotiwa kukaribia kumwajiri Mauricio Pochettino kama kocha wao mpya baada ya The Blues hao kuamua kumfukuza Graham Potter mwanzoni mwa Aprili. Umepita takribani mwaka mmoja tangu Todd Boehly & Clearlake Capital wachukue mikoba ya...

Uk. 12&13



# WACHEZAJI 10 WANAOPASWA KUACHWA SIMBA

Kiungo mkabaji wa Simba raia wa Burkina Faso, Ismael Sawadogo (katikati), akiwa uwanjani kuitumikia timu yake kwenye moja kati ya mechi za Ligi Kuu. Ni mmoja wa wachezaji anayetarajiwa kuachwa mwishoni mwa msimu baada ya kiwango chake kutomridhisha yeyote yule kwenye klabu hiyo.

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya klabu ya Simba kuondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya robo fainali kwa mara ya nne kwenye misimu mitano, wanachama na mashabiki wa timu hiyo sasa wamekuja juu wakitaka mabadiliko makubwa kwenye kikosi.

**Wakati ikitaka kufanya usajili huo, wapo wachezaji ambao wataachwa mwishoni mwa msimu na taarifa zinasema itaacha wachezaji wengi, kwani ina kikosi kizima ambacho hakiwezi kusaidia kikosi cha kwanza.**

Mwandishi wa Makala haya, ameorodhesha wachezaji 10 ambao wanatakiwa kuondoka na kupisha usajili wa wataokuja kuitoa hapa ilipo kwenda mbele.

**1. Habib Kyombo**

Alisajiliwa na kuanza kuitumika timu mwanzoni mwa msimu akitokea Mbeya Kwanza wakati huo ikiwa Ligi Kuu Tanzania Bara. Straika huyo alitegemewa kuchukua taratibu nafasi ya John Bocco ambaye umri imeanza kumtupa mkono, lakini hata akiingia haonyeshi chochote tofauti.

Ni mmoja wa wachezaji wanaotarajiwa kuonyeswa mlango la kutokea Msimbazi

**2. Mohamed Outtarra**

Beki huyu raia wa Burkina Faso kuelekea msimu huu akitokea Al Hilal ya Sudan akiwa tegemeo. Alitarajiwa kuziba vema pengo la Paschal Wawa aliyetimkia Singida Big Stars, lakini amekuwa akikaa benchi si kwenye michuano ya kimataifa tu, au ya Ligi Kuu, bali hata Kombe la FA. Huyu pia ni wa kuwapisha wachezaji wapya watakaosajiliwa.

**3. Gadiel Michael**

Alijiunga na Simba mwaka 2019 akiwa kama mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na Yanga. Tangu ajiunge hadi leo hajawahi kumtia wasiwasi Mohamed Hussein 'Tshabalala' kwenye namba yake ya beki wa kushoto. Kwa muda wote huo amekuwa mchezaji anayekuwapo uwanjani kama mwenzake ni majeruhi, au amepumzishwa kwa ajili ya mechi muhimu. Kama Simba inayokuja inataka wachezaji wawili wanaopigania namba eneo hilo, anapaswa aondoke. Amekuwa hachezeshwi hata kwenye michuano kama ya FA.

**4. Jonas Mkude**

Ndiye mchezaji pekee aliyehudumu muda mrefu kwenye kikosi cha Simba. Alikitumikia kikosi cha vijana chini ya miaka 20 hadi mwaka 2015 alipopandishwa kwenye kikosi cha kwanza na kuhudumu kwa misimu minane sasa.

Hata tangu msimu uliopita, kiungo huyo mkabaji hayupo kwenye kiwango chake cha kawaida. Anatajwa kuwa huu ni msimu wake ya mwisho, na anatakiwa awapishe wengine.

**5. Nassor Kapama**

Kapama ambaye ni anacheza nafasi nyingi uwanjani, tangu asajiliwe hajaonyesha cha ziada ambacho wanachama na mashabiki wa Simba wanakifikiria.

Alisajiliwa msimu huu kutoka Kagera Sugar na ingawa hucheza mara chache sana, lakini kiwango anachoonyesha ni cha timu za kawaida na si timu yenye mahitaji makubwa kama Simba.

**6. Augustine Okra**

Kuna wakati anakupa ambacho wanachama na mashabiki wa Simba wanakitaka, halafu kuna wakati hakupi. Hivi karibuni alitoka kwenye majeruhi. Na angalau alionyesha mchezo mzuri kwenye mechi dhidi ya Namungo Jumatano iliyopita. Hata hivyo inadaiwa ana mambo mengi nje ya uwanja na ndiyo inasababisha kutokuwa na mwendelezo mzuri. Kama Simba wanataka kufika nusu fainali msimu ujao, huyu pia anatakiwa aondoke.

**7. Erasto Nyoni**

Simba kama inataka kweli kuwafanya vema na kupita kwenye hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa haipaswi tena kuwa na mchezaji kama Erasto Nyoni. Siyo kama si mchezaji mzuri, lakini umri umemtupa mkono. Mwaka 2007 alikuwa anaichezea timu ya taifa, Taifa Stars akiwa anaichezea Vital'O ya Burundi. Ni miaka 16 sasa imepita, akiwa amepitia timu za Azam na Simba. Sidhani kama anweza kuendana na kasi ya wachezaji vijana kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Anafaa awapishe sasa vijana.

**8. John Bocco**

Itakuwa si vema kama Bocco hatotendewa haki kwa kuachwa kwa heshima mwishoni mwa msimu huu. Nahodha huyo ameifanyia vitu vingi vizuri Simba ikiwamo kuipa ubingwa misimu minne mfululizo. Kitendo cha viongozi kung'ang'ania aendelee si tu kama kinasababisha kuziba nafasi za kusajili vijana, lakini pia vijana wa sasa kumvunjia heshima yake anapokosea kwa sababu wao wanataka ushindi sio historia.

Inafaa naye aondoke au apewe kazi yoyote ile, ili nafasi yake ipate mtu mwingine damu changa ambaye anaweza kuitoa Simba hapo ilipo.

**9. Ismael Sawadogo**

Ni moja kati ya sajili mbovu zilizowahi kufanyika kwenye klabu hiyo. Na wala hakuna maneno mengi zaidi ya kusema tu awapishe wengine.

**10. Peter Banda**

Simba hajijawahi kumfaidi mchezaji huyo, na wale yeye hajawahi kuipa chochote zaidi ya kuvumiliana tu. Ni mchezaji kijana ambaye amekuwa akiandamwa na majeruhi, kila anapocheza mechi moja tu, iwe timu ya taifa yake ya Malawi au klabu yake.

Tangu asajiliwe msimu wa pili huu unaelekea ametumia muda mrefu kujiuguza kuliko uwanjani. Kwa sababu wachezaji wa kigeni wanatakiwa 12 tu na nafasi hizo ndizo zinatakiwa kusaka wachezaji bora watakaikwamua Simba, anatakiwa atolewe hata kwa mkopo kwenda kwenye timu nyingine kuliko kukaa na mchezaji ambaye klabu inatumia muda mwingi kumuuguza kuliko yeye kuitumikia timu uwanjani.

**JE, WAJUA?**

Baada ya timu ya Yanga kuifunga Singida Big Stars mabao 2-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara katikati ya wiki, ushindi huo umeifanya kufikisha pointi 71 na hivyo inahitaji pointi tatu ili ifikishe pointi 74 tu kujihakikishia taji hilo, kwa sababu hakuna timu yoyote inayoweza kufikia idadi hiyo. Simba iliyoko katika nafasi ya pili ina pointi 64 mkononi, endapo itashinda mechi zake tatu zilizobakia itafikisha pointi 73.





# Kamati Bunge yazuia kilimo Bwawa Mtera

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Maji na Mazingira, imeagiza wataalamu wa mazingira kuzuia wakulima kufanya shughuli za kilimo kando ya Bwawa la Mtera ili maji yasipungue.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jackson Kiswaga, aliyasema hayo jana kwenye ziara ya kamati hiyo ya kukagua Bwawa la Mtera ili kujiridhisha ujazo wa maji yaliyopo.

Kiswaga alisema wataalamu hao wana wajibu wa kutumia Sheria za Mazingira kuwazuia wakulima kufanya shughuli hizo kwa kuwa bwawa hilo ni chanzo muhimu cha maji na umeme.

"Lazima watu wa mazingira wafanye kazi yao kwa uhakika kwa sababu kinachofanyika watu wanaolima kandokando ya bwawa ni wavamizi na sheria haziruhusu lazima wachukuliwe hatua," alisema.

Alisema wasiposimamia sheria bwawa litaathirika na malengo ya kutoa maji kwenda Jiji la Dodoma hayatatimia kama maji hayo yasipolindwa.

"Fanyeni ukaguzi eneo la bwawa hili ili kuwabaini watu wanaovamia kufanya shughuli za kibinadamu, kama mnavyofahamu watu Dodoma wameongezeka kwa wingi baada ya serikali kuamua kuhamishia makao makuu hapa Dodoma, bwawa hili linatarajiwa kupeleka maji Dodoma," alisema.

Naye Waziri wa Maji, Jumaa aweso, alisema mahitaji ya maji ya Jiji la Dodoma ni lita milioni 133.4 kwa siku na ifikapo mwaka 2026 mahitaji yatafikia zaidi ya lita milioni 417.3 kwa siku.

"Chanzo kikuu cha maji kwa matumizi ya wakazi wa Jiji la Dodoma ni visima virefu vilivyochimbwa katika bonde la Makutupora eneo la Mzakwe," alisema.

Alisema miundombinu ya uzalishaji maji pamoja na uwezo wa usafirishaji maji ni lita milioni 61.5 kwa siku na

kuna vyanzo vingine vidogo kwa maeneo mahsusi ambavyo ni Ihumwa takribani lita milioni 5.6 kwa siku kwa ajili ya Mji wa Serikali, Iyumbu.

"Vyanzo vyote hivyo vinafanya uzalishaji wa maji kuwa jumla ya lita milioni 68.6 kwa siku, wakati mahitaji ya sasa mwaka 2022 ni lita milioni 133.8 kwa siku hivyo upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma ni lita milioni 65.2 kwa siku maji," alisema.

Alisema mipango iliyopo ya kuondoa tatizo la maji katika jiji hilo ni maji kutoka maji Ziwa Victoria, Bwawa la Farkwa na chanzo cha Bwawa la Mtera.




Balozi wa Uholanzi, Wiebe De Boer, akisalimiana na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati wa semina ya uendelezaji kilimo cha bustani, viazi na parachichi jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC abaini udhaifu utendaji kazi watumishi h'shauri

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amebaini kuwapo na udhaifu wa utendaji kazi kwa baadhi ya watumishi wa halmashauri za Mkoa wa Singida huku wengine wakiwa sehemu ya migogoro ya wananchi.

Serukamba alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akisikiliza kero za wananchi wa wilaya za Iramba, Mkalama, Singida, Ikungi na Manyoni ikiwa ni utaratibu aliojiwekea kila mwezi kusikiliza kero na kuipatia ufumbuzi.

Alisema watumishi wengine ni sehemu ya migogoro na kusababisha malalamiko kwa wananchi. Aliwataka watumishi hao kuepuka kuwa sehemu ya migogoro kwa wananchi kwa kutimiza wajibu wao, kusikiliza kero hizo na kuzitafutia ufumbuzi bila kujali ni ndogo au kubwa.

"Watumishi wenzangu tusiwe sehemu ya kero kwa wananchi...Tutekeleze majukumu yetu kwa kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi," alisema. Alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinajali wanyonge, na serikali ni lazima itekeleze majukumu yake kwa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua kwa kutenda haki pia kufanya vikao vya maridhiano.

Alisema wingi wa wananchi wenye kero wanaohudhuria vikao hivyo ni tafsiri tosha kuwa watumishi ngazi za chini hawatekelezi wajibu wao ipasavyo na kuagiza kila mtumishi kuwajibika katika eneo lake la kazi.

# Mhagama asisitiza ujenzi uendane thamani ya fedha

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, amewataka makandarasi wanaojenga majengo ya Mji wa Serikali kuendana na thamani ya fedha zilizopangwa.

Mhagama aliyasema hayo alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa majengo ya mji huo, Mtumba mkoani hapa.

Alisema pamoja na thamani ya fedha, makandarasi wanapaswa kuongeza kasi ya ujenzi ili yakamilike kwa wakati na kukidhi malengo ya serikali.

"Naomba muweke jitihada ili kuhakikisha mnakamilisha ujenzi kwa wakati fanyeni kazi kwa ushirikiano ili mtimize lengo mlilokabidhiwa na serikali," alisema Mhagama.

"Hakikisheni thamani ya fedha inaendana na mradi wa ujenzi wanaofanya serikali aihitaji kuona kuna ucheleweshwaji wa ujenzi huo."

Akiwa katika jengo la Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Waziri Mhagama aliwaasa makandarasi kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kutumia fursa ya ujenzi wa Mji wa Serikali kwa kufanya kazi kwa weledi jambo litakalosaidia kuuza ujuzi kwa wageni watakaotembelea mji huo.

Alisema wakifanya hivyo wageni wakija kutembelea eneo hilo, itawasaidia kuteka soko la nchi za Afrika Mashariki na nchi za kusini mwa Afrika kutokana na ujenzi bora watakaofanya.

Naye Msimamizi wa ujenzi wa jengo la wizara hiyo kutoka NHC, Mhandisi Aikani Mlekeo, aliishukuru serikali kwa kuwapa mwongozo mzuri katika usimamizi wa ujenzi wa mradi huo.





# ‘Marufuku kuuza ufuta kwa walanguzi’

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Songwe, imepiga marufuku wakulima wa ufuta wilayani humo kuuza zao hilo kwa walanguzi, badala yake litauzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kuanzia msimu huu.

Tangazo la kupiga marufuku hiyo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda, kupitia hotuba yake iliyosomwa na Ofisa Tarafa ya Ukukwe, Godwin Maungo, kwenye sherehe ya Siku ya Mkulima, Kata ya Chang’ombe wilayani hapa.

“Kuanzia msimu huu wa uuzaji wa ufuta, hakuna mkulima anayeruhusiwa kuuza ufuta kwa walanguzi na badala yake mtauza kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, huo ndiyo uamuzi wa serikali kwa sasa,” alisema Maungo.

Alisema uamuzi huo unalenga kumsaidia mkulima kupata bei nzuri ya mazao yake na kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya serikali yatokanayo na zao hilo.

Alisema kutokana na uamuzi huo hakuna mfanyabiashara binafsi anayeruhusiwa kuingia ndani ya wilaya hiyo kununua ufuta na akionekana atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Pia, alisema waliokubaliana kulipa ufuta kwa watu waliowakopesha wanaruhusiwa kuwalipa kama walivyokubaliana, lakini watakaolipwa hawaruhusiwi kwenda kuuza nje na badala yake wanapaswa kwenda kuuza kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Baadhi ya wakulima walisema uamuzi huo wa serikali ni mzuri na kuiomba kupata soko la uhakika ili kuepusha ufuta wao kukosa wanunuzi.

“Sisi wakulima tunahitaji kuuza mazao yetu kwa wakati na kwa bei nzuri, hivyo hatuwezi kupinga uamuzi wa serikali, lakini tunachoomba ni serikali kuhakikisha tunapata soko la uhakika,” alisema Masabila Mdelo, ambaye ni mkulima wa ufuta katika kijiji cha Chang’ombe.

Ofisa Kilimo Wilaya ya Songwe, Andrew Kapombe, alisema maandalizi ya maghala kwa ajili ya kununua ufuta kwa mfumo wa stakabadhi ghalani yamekamilika katika kila kijiji.

Alisema wakulima hao watauza ufuta wao kupitia kwenye vyama vyao vya ushirika (Amcos) ambavyo viko katika kila kijiji na kwamba vyama hivyo ndivyo vitakavyokuwa vikisimamia maghala hayo.



Mkurugenzi wa Shirika la Furaha ya Wanawake Wajasiriamali Viziwi Tanzania (FUWAVITA), Aneth Gerana, juzi alitoa mada ya namna gani watu wenye ulemavu, wanaweza kujikwamua kiuchumi bila kujali hali zao kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo wajasiriamali wenye mahitaji maalumu, yaliyofanyika kwenye Kanisa la Moravian Tanzania Ushirika wa Galilaya Mbalizi wilayani Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mapendekezo rasimu mpya sheria ukusanyaji mapato yapokewa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

UONGOZI wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, umepokea mapendekezo ya Baraza la Halmashauri ya wilaya hiyo kuhusu rasimu mpya ya sheria ya ukusanyaji wa mapato.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Missana Kwangura, ametoa kauli hiyo kwenye Baraza la Madiwani, miongoni mwa hoja zilizojadiliwa ni rasimu ya sheria mpya za ukusanyaji ushuru wa mazao ikiwamo mpunga.

Alisema katika majadiliano hayo, madiwani kwa umoja wao wamedai rasimu mpya sheria ya ukusanyaji mazao sio rafiki kwa wakulima na kupendekeza utumike mfumo wa zamani ambao ulikuwa na tija. “Madiwani wametoa ushauri kwamba rasimu ya sheria mpya ya ukusanyaji ushuru wa mazao sio rafiki kwa wakulima na wamependekeza urejeshwe mfumo wa zamani ambao ushuru ulikuwa unakusanywa kwenye mipaka ya kata na kata, lakini gunia moja kutozwa Sh. 1,000 badala ya 2,000 inayopendekezwa sasa,” alisema Kwangura.

“Mapendekezo haya tunayapeleka ofisi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa ajili ya kupitia upya mapendekezo haya ili kuruhusu mfumo walioupendekeza uanze kutumika.” Alisema baada ya kupokea mapendekezo hayo watayawasilisha kwa sekretarieti ya mkoa kwa ajili ya kufanya maamuzi ili kurejesha mfumo wa zamani ambao ulikuwa na tija na ufanisi wa ukusanyaji ushuru wa mazao.

Diwani wa Kata ya Rujewa, Michael Makao, alisema pamoja na mapendekezo ya kiwango za ukusanyaji wa mapato, pia wametaka ushuru huo usikusanywe tena na mawakala ili kuziba mianya ya rushwa, urudishwe kwa watendaji wa kata na vijiji.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, aliwataka watumishi na madiwani wilayani humo kila mmoja kutimiza wajibu wake kwa kuzingatia kanuni na sheria za utumishi ili kujiepusha na vitendo vya rushwa.

# Mbunge ashauri mikopo makundi maalum kuwapo mfumo riba nafuu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SIKU chache baada ya serikali kutangaza kusitisha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, ameshauri kuwapo na mfumo wa riba nafuu kwenye mkopo huo kwa kuwa umelenga kuyakwamua kiuchumi makundi hayo.

Alitoa maoni hayo baada ya maelekezo aliyoyatoa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, bungeni jijini Dodoma wakati alipohitimisha mjadala wa hoja ya makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Jimbo 2023/24, alizielekeza halmashauri kusitisha mikopo hiyo kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, mwaka huu.

Alisema hatua hiyo imechukuliwa ili kuipa fursa serikali ya kujipanga kuwa na mfumo mpya wenye tija wa kutoa mikopo, ikiwa na nia ya kuzihusisha Taasisi za Fedha ikiwamo benki ili ziweze kutoa mikopo kwa niaba ya halmashauri.

“Mikopo hii ilikuwa inatolewa bila riba na halmashauri, kwa bahati mbaya kuna baadhi ya watu wasio waaminifu wakawa wanakimbia sasa wakati serikali inatafakari kutumia njia za kibenki kutoa mikopo kwenye makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa niaba ya halmashauri ili kudhibiti kupotea kwa riba ni lazima sasa kuyawezesha makundi hayo kumudu kulipa mikopo hiyo ya fedha za umma,” alisema Suma Fyandomo.

Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Songwe, Juliana Shonza, aliwashauri kikundi hicho kuhakikisha wanachangamkia fursa zinazotolewa na halmashauri ili kufikia malengo yao.

“Licha ya serikali kubadilisha mfumo wa utoaji mikopo kwa nia ya kuwasaidia ni vyema sasa mkahakikisha mnapopatiwa mikopo hiyo mnairudisha kwa wakati ili kutoa nafasi kwa wengine kunufaika na fursa hiyo,” alisema Shonza.



# Zanzibar, India kuanzisha kampasi teknolojia ufundi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema imeingia makubaliano na Taasisi ya Teknolojia ya India kwa ajili ya kuanzisha kampasi itakayotoa mafunzo ya teknolojia ya ufundi na mawasiliano kwa wanafunzi kutoka Zanzibar.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa wizara hiyo, Lela Muhamed Mussa, wakati alipofanya mazungumzo na uongozi wa Taasisi ya Teknolojia ya India kupitia mwakilishi wake pamoja na balozi wa India aliopo nchini, Binaya Pradhan, Mazizini Unguja.

Alisema mikakati ya Wizara ya Elimu ni kuwapo kwa wahitimu zaidi katika fani ya ufundi wa teknolojia ya mawasiliano ambayo ndiyo mahitaji makubwa yaliyopo sasa.

Alisema kwa kuanzia ni muhimu kuwapo kwa tawi la chuo hicho nchini na kutoa mafunzo mbalimbali kwa vijana wenye fani ya teknolojia ya mawasiliano na ufundi.

Aidha, makubaliano hayo yanatarajiwa kufikiwa mwishoni mwa mwezi Mei na kampasi ya Chuo cha Teknolojia itaanza kutoa taaluma kuanzia mwezi wa Oktoba.

"Matarajio yetu kampasi ya chuo hicho kuanza kupokea wanafunzi na mambo ya taaluma katika mwezi wa Oktoba, mwaka huu ambapo sisi tutasimamia mambo ya utawala na wenzetu watatoa wahadhiri," alisema.

Akifafanua, alisema kuanzia jumla ya wanafunzi 50 kutoka Zanzibar watapata ufadhili wa masomo kwa ngazi ya shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu hali itakayongeza idadi ya wataalamu.

Balozi wa India, Binaya Pradhan, alisema wameamua kuanza kutoa masomo yao Zanzibar ikiwa sehemu ya hatua ya kuongeza ushirikiano na kutoa wataalamu katika fani mbalimbali.

"Alisema mahitaji ya wanafunzi wanaosomea masomo ya teknolojia ni makubwa duniani ambapo kwa upande wa India wamepiga hatua kubwa katika kusomesha na kutoa walimu katika fani hiyo," alisema.

Mwakilishi wa taasisi hiyo, Preeti Aghalayam, alisema wamejipanga kushirikiana na Serikali ya Zanzibar kuanzisha ushirikiano ambayo yatawezesha kupatikana kwa wanafunzi bingwa katika teknolojia ya habari na masuala ya ufundi.

# Benki yakabidhi wajasiriamali majiko sanifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya Diamond Trust (DTB), imekabidhi majiko sanifu rafiki kwa mazingira kwa wajasiriamali Zanzibar ambao wanajihusisha na shughuli za upishi.

Akizungumza jana katika hafla ya kukabidhi majiko hayo iliyofanyika Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Meneja wa benki hiyo tawi la Kijangwani, Amour Salim, alisema lengo la kutoa majiko hayo ni kuwainua wajasiriamali kiuchumi.

Alisema wajasiriamali wanachangamoto nyingi ikiwamo kutumia gharama kubwa katika uwezeshaji, majiko hayo yatasaidia katika uzalishaji.

"Majiko haya 32 tuliyatoa ni rafiki wa mazingira na yanatumia mafuta kidogo na wala hayatoi moshi wakati wa kupikia na gharama yake ni Shilingi milioni saba," alisema Amour. Alisema changamoto nyingine walizonazo wajasiriamali ni mitaji, benki hiyo imedhamiria kushirikiana na serikali kutimiza azma ya kuwainua ili kufikia malengo katika kukuza uchumi wa Zanzibar.

Alisema, wamelenga kundi la wanawake katika kuwapatia majiko hayo kwa sababu ndio wanaopata changamoto katika uchumi, licha ya kujituma, matunda hayaonekani.

Naye Mkurugenzi wa wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, Juma Burhan, alisema wajasiriamali kukuza biashara zao, wanahitaji kupatiwa elimu ya ufanyaji wa biashara na kutengenezewa mazingira mazuri ya kuweka akiba zao benki na kukua kiuchumi.

Aliipongeza benki hiyo kwa jitihada hizo zitakazowakomboa kiuchumi wajasiriamali hasa wanawake ambalo ni kundi kubwa lenye kipato duni.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhna Soraga, alipongeza benki hiyo kuiunga mkono serikali kuwasaidia wajasiriamali kuendesha ajenda ya wananchi kiuchumi.

Alisema wizara ipo pamoja na benki hiyo katika kila ushirikiano kwa sababu mahitaji ya wajasiriamali ni mingi uwezo unaporuhusu kutanua wigo wa kuwasaidia.

Waziri Soraga, alisema changamoto kubwa ya wajasiriamali ni elimu na biashara nyingi zinafeli ndani ya kipindi cha miaka miwili, zaidi ya asilimia 95 za biashara hufa katika kipindi hicho kwa sababu watu hawana ujuzi.

Aliwataka wajasiriamali hao kuwa makini katika mafunzo wanayopewa, kuvitunza vifaa wanavyopewa na kuwa wepesi kukubali wanafundishwa ili kujikomboa kiuchumi na kuondokana na hali ngumu ya umaskini.

"Hii ni bahati ama ni fursa ya kipekee ya mtu kusema anakupa elimu, ujuzi wa jinsi ya kufanya shughuli za ujasiriamali hivyo ni vyema kusikiliza kwa umakini mnayofundishwa," alisema Soraga.

Wajasiriamali waliokabidhiwa majiko hayo na kupewa elimu ya utumiaji, walisema kuwa majiko hayo watayatumia kwa ajili ya kukuza biashara zao ikiwamo ya kupika vyakula (mama lishe) na yamekuja muda muafaka wa kipindi cha mvua ambacho upatikanaji wa mkaa na kuni huwa mgumu.



Mjasiriamali Nazira Hassan akisikiliza maelekezo ya utumiaji wa jiko sanifu ambalo ni rafiki wa mazingira baada ya hafla ya kukabidhi majiko 34 yaliotolewa na Benki ya TDB katika hafla iliyofanyika Wizara ya Kazi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Mwanakwerekwe Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yafagilia mikopo kwa njia ya kidijitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya Salum, amesema mfumo wa mikopo kwa njia ya kidijitali itarahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo Zanzibar.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Juma Malik Akili, alitoa ujumbe huo kwa niaba ya waziri huyo wakati akifungua warsha ya kujadili mfumo wa kupata fedha kwa njia kidijitali uliohusisha taasisi za kifedha.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupata mikopo kwa wakati na kupanga harakati za maendeleo katika miradi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Alisema kutumia mifumo ya kidijitali katika njia ya mikopo itarahisisha kuokoa muda tafauti na ilivyo sasa.

Pia kwa kuwa dunia hivi sasa inakwenda na wakati na Zanzibar ni sehemu ya dunia, lazima kuwapo mabadiliko katika utendaji hasa ukopaji kwa kutumia TEHAMA kwa kuokoa muda wa kupata mikopo.

Mkuya alifafanua kuwa Zanzibar haikuwa ikitumia mfumo huo hali inayosababisha kutumia muda mrefu kupata fedha kwa wakati sahihi.

Alisema baada ya kufikiri na kuona ipo haja kutumia mfumo wa kidijitali katika kukopa kwenye taasisi za kifedha, serikali imeona ipo haja kuandaliwa na mkutano huo wa wadau kuona jinsi Zanzibar nayo itakavyonufaika na mfumo huo. "Serikali ya Zanzibar imeamua kujadiliana na wadau mbalimbali kutoka nje ya Tanzania ili kuona mfumo huo unavyokuwa na mafanikio," alisema.

Naye Mkurugenzi wa taasisi ya tafiti za mambo ya sera za kiuchumi Zanzibar, Juma Hassan Reli, alisema maendeleo ya mataifa mengi duniani yanakua kutokana na mifumo ya kifedha katika mfumo wa TEHAMA.

Baadhi ya taasisi za kifedha zilizoshiriki katika warsha hiyo zimesema zipo tayari kushirikiana na serikali hasa katika uwezeshaji wa mfumo kupitia matumizi ya TEHAMA na kurahisisha upatikanaji wa fedha hizo.

Mkutano huo wa siku mbili umehusisha washiriki kutoka wadau kutoka ofisi ya Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Sera za Uchumi Zanzibar, Ofisi ya Mkuu wa Serikali, Benki ya Watu wa Zanzibar pamoja na mamlaka ya kukuza uwekezaji.




Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai (katikati), akipokea funguo kutoka kwa Meneja wa Uwajibikaji kwa Jamii PanAfrican Energy an Orca Company, Andrew Kashangaki (kulia), kwa ajili ya kukabidhi majengo sita ya kituo cha afya yaliyojengwa na kampuni hiyo kwenye kijiji cha Chumo Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 800 juzi. Majengo hayo yatatoa huduma ya wagonjwa wa nje (OPD), chumba cha kuhifadhia maiti, maabara, kulazwa wagonjwa, kufulia nguo na upasuaji. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Farida Kikoleka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 1.1/- kumalizia maboma

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imetenga Sh. bilioni 1.1 kwa ajili umaliziaji wa maboma ya shule za msingi na ujenzi wa zahanati mpya tano.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Ally Machela, aliyasema hayo wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika Ukumbi wa Manispaa hiyo mwishoni mwa wiki.

Alisema kuwa kati ya fedha hizo, Sh. milioni 625 ni kwa ajili ya umaliziaji wa maboma na majengo ya utawala katika shule za msingi na sekondari.

Machela alisema kiasi kingine cha zaidi ya Sh. milioni 540 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati mpya tano katika baadhi ya kata zilizopo ndani ya manispaa hiyo.

"Tumejiwekea mipango mikakati katika bajeti yetu kwa kuanza na ujenzi na umaliziaji wa maboma ya shule za msingi na majengo ya utawala na pia kujenga zahanati tano mpya," alisema Machela.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha mwaka 2022, Halmashauri ya Manispaa ilikamilisha kujenga zahanati sita ambazo zilifunguliwa na zimepata watumishi na zinaendelea kupatiwa dawa, hivyo wananchi wanaendelea kupata huduma za afya.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha, zitajengwa zahanati mpya nyingine tano na katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu watakuwa na jumla ya zahanati mpya 11.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo alisema mbali ya ujenzi wa zahanati, pia watajenga vituo vya afya viwili - kimoja kinajengwa kutokana na fedha za mapato ya ndani na kingine ni fedha kutoka Serikali Kuu.

"Vituo hivyo tunatarajia kuvikamilisha muda wote na tukiwa na vituo vya afya viwili na zahanati 11 ndani ya manispaa. Huduma hii ya afya itakuwa imewafikia wananchi wetu kwa kiasi kikubwa," alisema Machela.

Akizungumzia umaliziaji wa maboma ya shule za msingi, alisema zimatengwa Sh. milioni 625 na baadhi zitakazoanza kumaliziwa maboma ni Shule za Msingi Tungi, Mafiga na Kilakala.

Mkurugenzi wa Manispaa huyo pia alisema kupitia mradi wa BOOST wa Serikali Kuu, fedha zitakapopokewa, utekelezaji wake utaanza mara moja kuzikamilisha shule zote zilizoainishwa.

Diwani wa Luhungo, Abdallah Chamgulu alisema upandaji miti katika Hifadhi ya Bwawa la Mindu umekuwa ukishirikisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa kisiasa, wananchi na wanaharakati wa mazingira.

Diwani wa Mbuyuni, Samweli Msuya aliutaka uongozi wa manispaa hiyo kuchukua hatua kwa wafanyabiashara walioacha vizimba na kwenda kupanga bidhaa pembezoni mwa Soko la Chifu Kingalu na kando ya barabara zilizopo ndani ya manispaa hiyo.

# Mwenyekiti UVCCM aonya viongozi wanaotafuna mali

**Na Suleiman Rashid Omar,**
PEMBA

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Kusini Pemba, Amina Abeid Mussa, amesema hatomvumilia kiongozi yeyote kuanzia ngazi ya tawi hadi jimbo anayejihusisha na ubadhirifu wa fedha au mali za wanachama wa chama hicho.

Akizungumza na wanachama wa UVCCM kutoka majimbo ya Mkoani na Mtambile huko Mkanyageni kisiwani hapa wakati wa ziara yake Mkoa wa Kusini, alisema kumekuwapo baadhi ya viongozi ambao wanajihusisha na ulaji wa fedha za wanachama.

Alisema tabia hiyo inarudisha nyuma maendeleo ya chama na kudhoofisha jitihada za vijana kujenga chama chao.

Mwenyekiti huyo alisema utafiti uliofanyika umegundua bado jumuiya za vijana Wilaya ya Mkoani hazijanufaika na fursa za mikopo inayotolewa na serikali katika kuwaendeleza vijana hao.

Viongozi walioshiriki mkutano huo waliwaomba viongozi hao wa mkoa kuhakikisha fursa za maendeleo zinawafikia vijana huku wakiahidi kutoa ushirikiano katika kuiimarisha CCM.

Katika ziara yake hiyo, kiongozi huyo alitembelea majimbo yote ya Wilaya ya Mkoani ambayo ni Mkoani, Mtambile, Kiwani na Chambani.

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 674/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU IMANI ZUBERI MARIJANI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA SHAZMIN SAID KIMARO**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 05 Mwezi wa 05 Mwaka 2023.

HAKIMU

# Airtel, IIT kupanua wigo wa teknolojia

**Na Halfan Chusi**

UONGOZI wa Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Airtel Tanzania umekutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa juu wa Taasisi ya Teknolojia ya India (IIT) kwa lengo la kupanua wigo wa masomo ya teknolojia ya mtandao nchini.

Huku IIT ikiwa tayari kuanzisha tawi lake nchini, Airtel Tanzania imejiandaa kutoa huduma bora za mawasiliano na huduma za data kwa taasisi hiyo inayoongoza kwa kutoa masomo ya teknolojia.

IIT ni moja ya taasisi maarufu duniani kwa teknolojia. Inatoa kozi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Metallurgy, Uhandisi wa Madini, Uhandisi wa Kemikali na zinginezo huku ikiwa na kampasi mbili tu nje ya India ambazo ziko Abu Dhabi na Kuala Lumpur. Mazungumzo hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki wakati uongozi wa juu wa IIT ulipotembelea makao makuu ya Airtel katika ziara ya kikazi iliyolenga kuangalia ni kwa jinsi gani IIT inavyoweza kusaidia elimu ya Tanzania na hasa kuhusu teknolojia.

Baada ya mazungumzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh, alisema ushirikiano huo mpya kati ya Airtel na IIT, unaunganishwa kwa kutoa huduma ya mawasiliano na huduma za data zenye kiwango bora baada ya kuanzishwa kwa tawi la chuo hicho Zanzibar. Litaitwa IIT Madras, likihudumia Zanzibar na maeneo mengine ya Ukanda wa Afrika Mashariki.

Balsingh alisema "IIT Zanzibar inatarajiwa kuanza kutoa masomo Oktoba 2023 huku ikiwa na kundi la kwanza la wanafunzi 50 wa shahada ya kwanza na wanafunzi 20 wa uzamili."

Balisngh alisema uamuzi wa kuanzisha kampasi yake ya kwanza Zanzibar umetokana umuhimu wa kihistoria wa visiwa hivyo na jitihada zake za sasa za kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha biashara cha kimataifa.

"Airtel Tanzania kwa muda mrefu imekuwa ikiunga mkono juhudi mbalimbali za serikali. Kwa sasa, serikali imekuwa inawekeza sana kwenye uanzishaji wa viwanda na kwa maana hiyo IIT ikaona umuhimu huu wa kutoa masomo ya teknolojia kwa wanafunzi wa kitanzania wakiwa nchini ili kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali yetu," alisema Balsingh.

## Urusi yailaani Ujerumani

**LONDAN,** UINGEREZA

MKUU wa kikundi cha Republic kinachoendesha kampeni dhidi ya kupinga utawala wa kifalme Graham Smith, amekamatwa akiwa kwenye maandamano katika eneo la Trafalgar kabla ya shughuli ya kutawaza kwa Mfalme Charles III.

Inaelezwa kuwa vipande vya video vinaonyesha jana waandamanaji waliovaa fulana zilizoandikwa maandishi yanayosomeka 'Not My King' wakizuiliwa, akiwamo Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa kikundi hicho Smith.

Pia inaelezwa kuwa waandamanaji wengine sita akiwemo Smith, walikamatwa na polisi walipokuwa wakipakua mabango karibu na njia ya msafara wa kutawazwa kwa mfalme.

Republic ilichapisha picha za maofisa wakichukua maelezo kutoka kwao kwenye ukurasa wao wa Twitter.

Kikundi hicho kilisema wana haki wa kuandamana kwa amani, na kwamba maofisa hao hawatatoa sababu za kukamatwa kwao na kuthibitisha Mkurugenzi Mtendaji wao alikuwa miongoni mwao.

Matt Turnbull, ambaye ni mmoja wa waliokamatwa, alisema kuwa maandamano yao yalieleweka vibaya, na kwamba yalionekana kama kitu ambacho kingeweza kutumika kuzuia kilichokuwa kinaendelea.

"Kusema kweli hatukuwahi kuruhusiwa na nguvu inayoonekana hapa walijua tunakuja, na wangetafuta njia ya kukomesha hili," alisema Turnbull.

Kwa mujibu wa BBC, muda mchache baada ya kiongozi huyo kukamatwa, baada ya muda alionekana akitolewa nje huku akiwa amefungwa pingu.

Aidha, inaelezwa kuwa wakati hayo yakiendelea polisi bado hawajathibitisha idadi kamili ya watu waliozuiliwa, zaidi ya kusema watu kadhaa walikamatwa karibu na njia ya gwaride la kutawazwa kwa mfalme.

Inabainishwa kuwa maandamano ya kupinga ufalme yalipangwa karibu na Trafalgar Square katikati mwa London, huku umati wa watu wakiimba nyimbo za 'Not my King' na 'Free Graham Smith.

Pia ilielezwa kuwa maelfu ya watu walikusanyika kutazama msafara wa kutawazwa kwa mfalme kutoka kasri la Buckingham hadi Westminster Abbey kabla ya sherehe. **BBC**

## 7 wauawa, 22 wakitekwa nyara Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

VYANZO vya usalama nchini Nigeria vimesema watu saba wameuawa huku wengine 22 wakitekwa nyara katika mashambulizi mawili tofauti yaliyotokea katika jimbo la kaskazini mashariki la Borno, mahala ambako makundi ya wanajihadi yanaendesha harakati zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na vyanzo hivyo jana, ukosefu wa usalama ni wasiwasi mkubwa katika taifa hilo lenye watu wengi barani Afrika wakati Rais mpya akitarajiwa kuapishwa mwezi huu baada ya kushinda uchaguzi ulioibua utata kutoka kwa upinzani.

Pia ilibainishwa kuwa Alhamisi ya wiki iliyopita, wakulima watatu waliuawa na 11 wengine walitekwa nyara na wanaoshukiwa kuwa ni wanajihadi wa Islamic State West Africa Province (ISWAP) karibu na kijiji cha Bulayobe kuelekea mji wa Banki.

Vyanzo vya ndani vilisema wakulima waliingia kilomita 10 nje ya Banki kusafisha mashamba kwa ajili ya maandalizi ya msimu wa kupanda mazao wakati mvua za kila mwaka zikitarajiwa baada ya siku kadhaa. **VOA**

# UN yahimiza juhudi ziongezwe kurudisha amani Congo DR

**KINSHASA,** DRC

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amewahimiza viongozi wa ngazi za juu wa Afrika kuongeza juhudi katika kutafuta suluhu ya mgogoro unaoendelea Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ili kurejesha amani.

Guterres aliyasema hayo mwishoni mwa juma lililopita wakati alipokuwa akihutubia katika mkutano wa ngazi ya juu ya mataifa ya Afrika uliofanyika nchini Burundi, na kwamba mataifa hayo yalitia saini makubaliano ya UN ya mwaka 2013 kwa ajili ya kuhamasisha utulivu.

Alisema makubaliano yaliyoanzishwa muongo mmoja uliopita yaliashiria mabadiliko ya ushirikiano katika eneo linalokumbwa mara kwa mara na matatizo, lakini mgogoro uliopo sasa unaelezea namna wanavyopaswa kusonga mbele.

"Licha ya juhudi zetu za pamoja, zaidi ya makundi mia moja yenye silaha yalipo ndani ya DCR na nje bado yanaendesha harakati hivi leo na hivyo kutishia uthabiti wa eneo zima la Maziwa Makuu," alisema Guterres.

Guterres pia alihutubia mkutano wa marais na viongozi waandamizi wengine akiwa mjini Bujumbura. **VOA**



Kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, akionekana nyumbani kwa Mchungaji Pasta Ezekiel Odero, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Saudi Arabia kuwakutanisha mahasimu wa Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

SAUDI Arabia itakuwa mwenyeji wa mazungumzo ya kwanza ya ana kwa ana kati ya makundi mawili ya kijeshi yanayopigana nchini Sudan wakati huu mapigano yakiendelea kuripotiwa nchini humo licha ya kuwapo kwa wito wa kusitishwa.

Hatua hiyo ya Saudi Arabia inakuja wakati huu pia makubaliano ya awali yalioafikiwa na pande hizo hasimu za kijeshi ya kusitisha mapigano yakionekana kutibuka kwa mara kadhaa.

Kwa mujibu wa taarifa ya pamoja kutoka kwa nchi za Marekani na Saudia Arabia imeeleza kuwa kukaribisha kile imetaja kuwa majadiliano ya kabla ya mazungumzo huko Jeddah kati ya jeshi la Sudan na vikosi maalum vya RSF.

Mkutano huo wa kujaribu kupata suluhu ya kinachoendelea nchini Sudan unakuja wakati mapigano yakiendelea kuripotiwa katika baadhi ya miji nchini humo ikiwamo jiji kuu la Khartoum.

Kwa mujibu wa jeshi la Sudan, mazungumzo hayo yanalenga masuala muhimu yanayoibuka haswa suala la kibinadamu, huku ikielezwa kuwa idadi kubwa ya raia nchini Sudan wameendelea kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa chakula na maji kutokana na mapigano hayo.

Hata hivyo, wananchi wengi wa Khartoum walieleza kukabiliwa na changamoto hizo, wakisema kuwa hawawezi kutoka nje kwenda kutafuta bidhaa hizo muhimu kwa kuhofia kushambulia.

Tayari jeshi la Sudan limethibitisha kuwatuma wajumbe wake mjini Jeddah kushiriki katika mazungumzo hayo, japokuwa vikosi vya RSF kwa upande wake havijatoa taarifa yoyote kuhusu suala hilo.

Umoja wa Mataifa (UN) na mashirika ya misaada yamekuwa yakieleza kuwa huenda raia nchini humo wakakabiliwa na mzozo wa kibindamu iwapo mapigano hayo yataendelea.

Vile vile, inabainishwa kuwa watu zaidi ya 400 wamethibitishwa kufariki katika mapigano hayo ya wiki tatu sasa, huku wengine zaidi ya 400,000 wakiripotiwa kuyakimbia makazi yao.

Mataifa jirani na Sudan kama vile Chad na Sudan kusini yameripoti kuwapokea mamia ya raia wa Sudan wanaokimbilia katika mataifa hayo kutafuta hifadhi. **RFI**

# PAMBA, KITAYOSCE VITA KUBWA CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Pamba ya Mwanza na Kitayosce ya Tabora zimezidi kung'ang'ania kooni kwa ajili ya kusaka nafasi moja iliyobaki ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara moja kwa moja, baada ya zote mbili kushinda mechi zao juzi.

**Wiki iliyopita timu hizo zote zilitoa sare kwenye mechi zao zilizocheza.**

Kitayosce, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Ally Hassan Mwinyi, Tabora iliifunga Mbuni FC bao 1-0, lililowekwa ndani ya wavu dakika ya sita tu ya mchezo na straika Mkongomani, Fabrice Ngoy wa Ngoy ambalo lilidumu hadi mwisho wa mchezo.

Matokeo hayo yanaifanya Kitayosce kubakisha mechi moja tu kabla ya kuhitimisha mechi zake kwenye Ligi ya Championship ikishika nafasi ya pili kwa pointi 57, chini ya JKT Tanzania ambayo tayari imeshamaliza mechi zake na imepanda Ligi Kuu ikiwa na pointi 63.

Pamba ikiwa kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza, ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania na kuendelea kung'ang'ania nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi ya Championship kwa pointi 56, moja nyuma ya Kitayosce. Bao pekee la washindi lilifungwa dakika nane kabla mechi kumalizika na William Kisingi.

Timu zote hizo mbili zimebakisha mechi moja na atakayemaliza nafasi ya pili ataungana na JKT Tanzania kupanda moja kwa moja na itakayobaki itakwenda kucheza mechi za mchujo na timu za Ligi Kuu.

Wakati huo huo, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania imepokea barua ya maombi kutoka klabu ya Ndanda ya mkoani Mtwara wakiwasilisha maombi yao ya kujitoa kwenye Ligi ya Championship msimu wa 2022/23 kwa kile walichoeleza kuwa ni kutokana na changamoto ya kifedha.

Klabu hiyo ilishindwa kusafiri kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya mechi namba 230 ya Ligi ya Championship dhidi ya Pan African uliopangwa kucheza Mei 6 kwenye Uwanja wa Uhuru.

Kwa maelezo hayo, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania inatangaza kuwa mchezo huo hautokuwapo na taarifa itapelekwa kwenye Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi kwa ajili ya kujadiliwa, kisha kutolewa maamuzi.




Mshindi wa nne wa mbio za Absa Dar City Marathon, Oscar Shananga (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga, baada ya mashindano hayo jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Obedi Laiser. Benki ya Absa ilikuwa mdhamini mkuu wa mbio hizo ikitoa kiasi cha Sh. milioni 45. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ligi ya Soka Wanawake Arusha yaanza

**Na Adam Fungamwango**

LIGI ya Soka Taifa Wanawake mkoani Arusha imeanza kutimua vumbi juzi kwenye viwanja vinne ikizishirikisha jumla ya timu 15.

Kwa mujibu wa chama cha soka mkoani Arusha (ARFA) ligi hiyo inachezwa kwa mgawanyo wa makundi yaliyogawanyika mara nne, huku kila kundi likitegemea kupata mshindi mmoja atakayecheza moja moja nusu fainali.

Kundi A limatajwa kuwa na timu za Arusha Sekondari, Kaloleni Sekondari, na Arusha Day, huku Kundi B likiwa na timu za King Youth Queens, Lemara Sekondari, Sinoni Sekondari na Edmund Sekondari.

Timu zilizowekwa Kundi C ni St Jude, Kimaseki, Elct Usariver Cys Centre na Suye, Kundi D ikiwakilishwa na timu za Elerai Sekondari, Olasit Sekondari, Muriet Sekondari na Intel School.

ARFA, imesema viwanja vitakavyotumika kwenye ligi hiyo ni Sinoni ambao utatumika kwa timu zilizo Kundi D, Kundi C linacheza mechi zake kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha Sekondari utatumika kwa timu zilizo Kundi B, na FFU kwa Mrombo utatimua vumbi kwa timu za Kundi A.

Taarifa ya ARFA imesema kila kundi itatoa mshindi mmoja na kuwa jumla ya timu nne zitakazocheza hatua hiyo kwa ajili ya kusaka timu zitakazopanda kwenda Ligi Daraja la Pili.

Wakati huo huo, Ligi ya TFF wanawake nchini ya miaka 20 mkoani Dar es Salaam iliendelea juzi, Temeke Sisters ikisulubiwa mabao 3-0 dhidi ya Young Stars na Tanzanite Princess ikiichapa Ubungo TFSEO bao 1-0, mechi zote zikipigwa kwenye Uwanja wa Karume, Ilala jijini Dar es Salaam.

## KMKM bado haina uhakika na ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, amesema licha ya kupata ushindi katika mchezo wao dhidi ya JKU bado wanahitaji kupambana zaidi ili kuhakikisha wanafanikiwa kutetea Ubingwa wa Ligi Kuu Zazibar msimu huu.

KMKM juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya JKU katika mwendelezo wa ligi hiyo ikiwa mzunguko wa lala salama.

Ushindi huo umeifanya KMKM kufikisha alama 57 katika michezo 26 walizocheza wakiendelea kuchuana vikali na wapinzani wao KVZ wenye alama 53 huku wakiwa wamecheza michezo 25.

Alisema licha ya kubakia michezo minne ya kumaliza ligi bado mapema kusema kama wanamwelekeo wa ubingwa kutokana na wapinzani wao kuwafuata kwa karibu.

Alisema mioyo yao inaendelea kuwa na matumaini ya kutetea taji lao hilo, lakini jitihada zaidi zinahitajika ili kuona wanafanikiwa.

Aidha alisema kikosi chao kinaendelea kujifua ili kuhakikisha kinafanya vizuri kwenye michezo minne iliyobaki ili kutetea ubingwa wao.

## Majiha kupanda ulingoni Juni 30

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa Tanzania, Fadhili Majiha 'Stopper' anatarajia kupanda ulingoni Juni 30, mwaka huu katika pambano ambalo Mfaume Mfaume atacheza na Nkululeko Mhlongo raia wa Afrika Kusini kwenye pambano kuu.

Pambano hilo ambalo limeandaliwa na PAF Promotion Entertainment Company LTD linatarajia kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Fadhili Maogola alisema tayari washamalizana na Majiha kwa ajili ya kucheza pambano hilo na kwa sasa wanajipanga kumalizana na mpinzani wake ambaye bado hajawekwa wazi.

"Hakuna ambaye hajui ubora na ukubwa wa Majiha akiwa ni bondia anayekamata nafasi ya pili katika mabondia bora Watanzania kwa sasa, kilichobakia kwa sasa, tunaweka mipango na mikakati yetu vizuri na kuweza kumalizana na mpinzani wake," alisema Mkurugenzi huyo.

Alisema hawawezi kuweka wazi jina la mpinzani wa Majiha kwa sababu ya mambo ya kibiashara hadi watakapokuwa wamemalizana kwa kusaini mkataba kwa ajili ya pambano hilo.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## PHILLIPS, WALKER WATAKIWA

KLABU ya West Ham inataka kuwasajili kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips, 27 na beki wa kulia Kyle Walker, 32. ***(90min)***

## MESSI ATAJWA UARABUNI

MSHAMBULIAJIA wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi, 35, amehusishwa na kuhamia klabu ya Saudi Arabia Al Hilal - uhamisho ambao utamfanya mshambuliaji wa Nigeria, Odion Ighalo, 33, kuondoka katika klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

## GUIMARAES MKATABA MPYA

KIUNGO wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes, 25, anatazamiwa kusaini mkataba mpya na Newcastle United ambao utamfanya kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika historia ya klabu hiyo. ***(Football Insider)***

## JUVE YAMTAKA GREENWOOD

KLABU ya Juventus inataka kumsajili mshambuliaji wa England, Mason Greenwood, 21, kwa mkopo kutoka Manchester United. ***(Sun Sunday)***

## MOUNT ANASAKWA

KIUNGO wa kati wa Chelsea na England, Mason Mount, 24, anasakwa sana na Liverpool. ***(Mail Sunday)***

## ALLISTER ANAITAMANI LIVER

KIUNGO wa kati wa Brighton, Alexis Mac Allister, 24, ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na Argentina, "anatamani sana" kujiunga na Liverpool. ***(Football Insider)***

## RAPHINHA NA BARCA

WINGA wa Brazil, Raphinha, 26 anafikiria kuondoka Barcelona msimu huu wa joto. Arsenal wanamtaka mchezaji huyo wa zamani wa Leeds United, huku Chelsea na Newcastle United pia zikimtaka. ***(Sport)***

## SPURS KULIPA FIDIA

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikalazimika kulipa Bayern Munich pauni milioni 10 kama fidia ili kumpata Julian Nagelsmann kuwa kocha wao mkuu mpya. ***(Sunday Telegraph)***

## ALONSO CHAGUO KUU

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso ndiye chaguo kuu la mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy. ***(Mirror)***

## SABITZER BADO

KIUNGO wa kati wa Austria, Marcel Sabitzer, 29, bado hajafanya mazungumzo kuhusu mustakabali wake na kocha wa Bayern Munich, Thomas Tuchel. Sabitzer kwa sasa yuko kwa mkopo Manchester United. ***(Sky Germany, via Manchester Evening News)***

## BENNACER AWANIWA

MANCHESTER City na Arsenal zote zinataka kumsajili kiungo wa kati wa AC Milan na Algeria, Ismael Bennacer, 25. ***(FootballTransfers)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LAMPARD: WACHEZAJI SASA MNAWEZA KUNYWA MVINYO

●●● Baada ya Chelsea kupata ushindi wa kwanza kwa michezo sita, huku yeye akiongoza...

**LONDON,** England

FANK Lampard aliwahimiza wachezaji wake kusherehekea kwa bia au glasi ya mvinyo baada ya Chelsea kupiga "hatua ndogo mbele" kusitisha mfululizo wao wa kupoteza mechi sita kwa ushindi wa 3-1 dhidi ya Bournemouth, Jumamosi.

**Mabao ya dakika za lala salama kutoka kwa Benoit Badiashile na Joao Felix yaliwapatia The Blues ushindi uliochelewa baada ya beki wa Cherries hao, Matias Vina kufuta bao la mapema la Conor Gallagher kwenye Uwanja wa Vitality.**

Mafanikio hayo aliyoyapata kwenye pwani ya kusini yalikuwa ya kwanza kwa Lampard tangu arejee Stamford Bridge kwa muda wa mwezi mmoja uliopita na njia muafaka ya kufikisha mechi yake ya 100 kwenye ukocha katika Ligi Kuu ya England.

Kiungo huyo wa zamani wa England na Blues aliitaka timu yake kukumbatia ushindi huo wa kwanza wa klabu hiyo ndani ya takriban miezi miwili, lakini akaonya kwamba lazima wajipande katika mechi zao nne za mwisho za msimu huu mbaya.

"Wanapaswa kufurahia na tunafurahi kwa sababu wakati huu una hisia hiyo na hatuna namna kwa sasa," alisema Lampard.

"Ilionekana wazi kwenye chumba cha kubadilishia nguo kutokana na kwamba kulikuwa na mambo mengi ambayo yalihitaji kufanywa na kwa bahati mbaya unahitaji matokeo ili kuendana na hayo ili kukufanya uendelee mbele.

"Leo (juzi) ilikuwa hatua ndogo nzuri mbele.

"Wavulana wote ni wanadamu, sote tunaathiriwa kwa njia zinazofanana wakati haushindi michezo au hujisikii kama uko katika ubora wako na njia pekee ya kushinda hilo ni kupigana na kufanyia kazi.

"Nimekuwa katika nyakati ngumu, kwa hiyo wanapaswa kufurahia usiku wa leo (juzi) na kunywa bia au glasi ya mvinyo au kufanya chochote wanachofanya.

"Lakini hatuwezi kuchukua hatua katika suala la kujaribu kupiga hatua hadi mwisho wa msimu huu kwa sababu ni muhimu."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 575,

MECHI KALI
BRIGHTON
VERSUS
EVERTON
1 | 1.35
X | 4.89
2 | 6.99

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SALAH ATAKA KUWEKA REKODI ZAIDI



**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah anataka kuweka rekodi baada ya bao lingine la kihistoria kuipata ushindi wa 1-0 dhidi ya Brentford, kwenye Ligi Kuu, Jumamosi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri alifunga bao la dakika ya 13 likiwa la 30 msimu huu - ikiwa ni mara ya nne kufikisha idadi hiyo ya mabao na bao lake la 100 akiwa Anfield.

Alikuwa mchezaji wa kwanza wa Liverpool kufunga katika mechi tisa mfululizo za nyumbani na kwa kufanya hivyo alifikia rekodi ya Steven Gerrard katika nafasi ya tano kwenye orodha ya wafungaji wa muda wote wa klabu akiwa na mabao 186.

"Ina maana kubwa kwangu. Nilisema hapo awali, ninahisi (niko) nyumbani hapa, nina furaha," alisema Salah akiambia Sky Sports.

"Ni kitu ambacho kinanifanya nijivunie, kuwa mwadilifu. Ninafanya kazi kwa bidii na kila mtu anajua hilo, kila mtu analiona hilo.

"Nimehamasishwa tu kuweka rekodi na kufunga mabao na michezo ya ushindi kwa timu."

Kwa upande wake, Kocha Jurgen Klopp alitoa sifa nyingi kwa kuhusu ubora wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

"Namba anazotengeneza, sote tunajua kwamba baada ya kazi yake ataonekana kama mmoja wa magwiji wa wakati wote, hiyo ni wazi," alisema bosi huyo wa Wekundu hao.

"Lakini sasa bado yuko kwenye kazi na watu wengine wanaweza kutomthamini vya kutosha, lakini tunafanya hivyo.



## *Pep akataa kuwakosoa Haaland, Gundogan*

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola alikataa kuwakosoa Ilkay Gundogan na Erling Haaland kwa kukosa penalti katika ushindi mwembamba usiotarajiwa wa Manchester City wa 2-1 dhidi ya Leeds United, Jumamosi.

Mpigaji wa mara kwa mara wa penalti, Haaland alimwachia Gundogan wakati City ilipozawadiwa mkwaju huo kwenye Uwanja wa Etihad ili kumwezesha Mjerumani huyo kukamilisha hat-trick.

Hata hivyo, Gundogan alikosa penalti hiyo iliyotoka kwenye nguzo ya mkono wa kushoto wa golikipa Joel Robles na Rodrigo akafunga bao la kufutia machozi kwa Leeds ambao inapambana kuepuka kushuka daraja.

Guardiola alionekana kukasirishwa sana wakati huo na alinaswa na kamera akisema anahisi Haaland, ambaye hakuongeza bao 51 angefunga penalti hiyo.

Guardiola alisem
"Uchezaji ulikuwa bor
tulicheza vizuri sana.

"Sitaelezea hisia za
gu kuhusu dakika tan
sita au saba zilizopi
kwa sababu kwa ujum
ilikuwa nzuri sana.

"Nani anajua kan
Erling alikuwa amepig
penalti na kukosa? Ni
kitatokea ikiwa Riya
(Mahrez) ataichukua n
kuikosa? Nini kitatoke
ikiwa Ilkay Gundoga
atapiga penati na k
funga?

## HABARI MICHEZO


# 472,890

## JACKPOT

Lorem ipsum

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 10/05/23 | 22:00 | AC Milan vs nter | 2.96 | 3.01 | 2.39 |
| 02. 11/05/23 | 01:00 | Coquimbo vs Univ de Chile | 2.58 | 3.32 | 2.43 |
| 03. 11/05/23 | 02:00 | Rangers vs San Luis Quillota | 2.64 | 3.00 | 2.58 |
| 04. 11/05/23 | 02:00 | FC Cincinnati vs New York City | 2.24 | 3.47 | 2.74 |
| 05. 11/05/23 | 03:30 | Cruzeiro vs Fluminense | 2.83 | 3.22 | 2.29 |
| 06. 11/05/23 | 05:30 | LA Galaxy vs Seattle Sounders | 2.44 | 3.21 | 2.64 |
| 07. 11/05/23 | 16:00 | Pontedera vs AC Siena | 2.37 | 2.78 | 3.04 |
| 08. 11/05/23 | 19:00 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.72 | 3.39 | 2.23 |
| 09. 12/05/23 | 01:00 | Coritiba vs Vasco da Gama | 2.40 | 3.17 | 2.72 |
| 10. 12/05/23 | 01:00 | Botafogo RJ vs Corinthians | 2.14 | 3.21 | 3.12 |
| 11. 12/05/23 | 01:00 | Univ de Concepcion vs Antofagasta | 2.85 | 2.96 | 2.43 |
| 12. 12/05/23 | 13:30 | FC Tokyo vs Kawasaki Frontale | 2.83 | 3.19 | 2.26 |
| 13. 12/05/23 | 19:00 | Slaven Belupo vs Lokomotiva Zagreb | 2.51 | 3.09 | 2.57 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 08/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3411 | Welayta Dicha FC vs Adama City FC | 2.60 | 2.70 | 2.60 |
| 17:00 | 1000 | Lokomotiv Moscow vs Sochi | 1.98 | 3.56 | 3.30 |
| 17:00 | 1074 | Preston vs Sunderland | 3.64 | 3.49 | 1.89 |
| 17:00 | 1648 | Birmingham vs Sheffield Utd | 3.60 | 3.40 | 1.93 |
| 17:00 | 2609 | Luton Town vs Hull City | 1.60 | 3.81 | 4.91 |
| 17:00 | 3190 | Middlesbrough vs Coventry | 2.35 | 3.34 | 2.74 |
| 17:00 | 3486 | Swansea vs West Bromwich | 2.95 | 3.40 | 2.19 |
| 17:00 | 4326 | Fulham vs Leicester | 2.56 | 3.32 | 2.51 |
| 17:00 | 4530 | Millwall vs Blackburn | 1.89 | 3.55 | 3.60 |
| 17:00 | 4660 | Wigan vs Rotherham | 2.26 | 3.45 | 2.80 |
| 17:00 | 5230 | Norwich City vs Blackpool | 1.47 | 4.20 | 5.80 |
| 17:00 | 5539 | Burnley vs Cardiff | 1.32 | 4.80 | 8.01 |
| 17:00 | 5691 | Watford vs Stoke City | 2.30 | 3.29 | 2.84 |
| 17:00 | 5703 | QPR vs Bristol City | 2.31 | 3.41 | 2.76 |
| 17:00 | 5776 | Huddersfield vs Reading | 1.99 | 3.35 | 3.45 |
| 18:00 | 4087 | ES Hammam Sousse vs EO Sidi Bouzid | 1.87 | 2.92 | 4.31 |
| 18:00 | 4511 | Fasil Kenema vs Arba Minch Kenema | 1.98 | 3.00 | 3.83 |
| 18:00 | 5888 | Ohud Medina vs AL Riyadh | 3.49 | 3.13 | 1.98 |
| 19:00 | 1421 | Al-Sailiya SC vs AL Wakrah | 2.93 | 3.55 | 2.06 |
| 19:00 | 1740 | Karabakh vs Gabala | 1.28 | 4.99 | 8.52 |
| 19:00 | 2859 | Umm-Salal SC vs Qatar SC | 2.36 | 3.23 | 2.66 |
| 19:00 | 3592 | Al Nasr Riyadh vs Al Khaleej Club | 1.20 | 6.18 | 12.79 |
| 19:00 | 5225 | AL Adalh vs Al Wehda | 2.36 | 3.35 | 2.87 |
| 19:30 | 1876 | Udinese vs Sampdoria | 1.49 | 4.09 | 5.79 |
| 19:30 | 2202 | Empoli vs Salernitana | 2.22 | 2.94 | 3.34 |
| 19:30 | 2373 | Brighton vs Everton | 1.35 | 4.89 | 6.99 |
| 20:00 | 1499 | Verl vs Osnabruck | 3.43 | 3.69 | 1.93 |
| 20:00 | 1893 | Orgryte IS vs Osters IF | 3.25 | 3.36 | 2.15 |
| 20:00 | 2285 | Pecs MFC vs MTK Budapest | 3.18 | 3.28 | 2.04 |
| 20:00 | 2507 | Brommapojkarna vs IFK Goteborg | 2.77 | 3.18 | 2.30 |
| 20:00 | 2518 | Galatasaray vs Basaksehir | 1.43 | 4.41 | 6.30 |
| 20:00 | 2666 | Sirius FK vs Elfsborg | 3.40 | 3.45 | 1.90 |
| 20:00 | 2840 | Brann vs Sandefjord | 1.23 | 5.68 | 10.31 |
| 20:00 | 2901 | Degerfors vs Norrkoping | 2.68 | 3.24 | 2.34 |
| 20:00 | 4512 | Trabzonspor vs Ankaragucu | 1.85 | 3.56 | 3.77 |
| 20:00 | 5877 | IK Brage vs GIF Sundsvall | 1.91 | 3.56 | 3.77 |
| 20:10 | 2585 | Djurgardens IF vs Kalmar | 1.78 | 3.39 | 3.96 |
| 20:30 | 2022 | Maccabi Haifa vs Maccabi Tel Aviv | 2.22 | 3.28 | 2.82 |
| 20:30 | 5847 | FC Ashdod vs Hapoel Beer Sheva | 4.73 | 3.70 | 1.59 |
| 21:00 | 1205 | Jong Ajax vs ADO Den Haag | 2.49 | 3.60 | 2.41 |
| 21:00 | 3439 | Famalicao vs GD Chaves | 1.98 | 3.32 | 3.57 |
| 21:00 | 4157 | Jong PSV vs PEC Zwolle | 5.11 | 4.38 | 1.49 |
| 21:00 | 4623 | Jong AZ Alkmaar vs FC Oss | 1.52 | 4.27 | 4.90 |
| 21:00 | 4916 | Jong Utrecht vs Den Bosch | 1.92 | 3.59 | 3.38 |
| 21:30 | 2354 | Al Ittihad Jeddah vs Abha | 1.23 | 5.74 | 11.70 |
| 21:45 | 1894 | Le Havre vs Rodez Aveyron | 1.76 | 3.40 | 4.40 |
| 21:45 | 4937 | Sassuolo vs Bologna | 2.31 | 3.35 | 2.80 |
| 22:00 | 1201 | Eibar vs Las Palmas UD | 2.13 | 3.00 | 3.50 |
| 22:00 | 5258 | Nottingham vs Southampton | 2.08 | 3.36 | 3.21 |
| 23:15 | 3885 | FC Arouca vs Porto | 7.25 | 4.73 | 1.36 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NAMUNGO FC NGUVU ZOTE KWA AZAM

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kutoka sare ya bao 1-1 na Simba kikosi cha Namungo FC sasa kimeelekeza nguvu zake kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC Juni 13 mwaka huu, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, kutoka mkoani Lindi Kocha Mkuu wa timu ya Namungo, Denis Kitambi, alisema mara baada ya kumalizana na Simba aliwapa wachezaji wake mapumziko ya muda mfupi ili kupumzisha miili yao.

"Niliwapa mapumziko ya muda mfupi wachezaji wangu hadi Jumamosi na sasa tumeanza maandalizi ya mchezo wetu tutakaoucheza ugenini dhidi ya Azam FC," alisema Kitambi.

**Kocha huyo alisema mapungufu kwenye safu yake ya ushambuliaji ambayo ilikuwa inampasua kichwa kwa sasa yamepungua na safu hiyo inaonekana kuimarika.**

Alisema hali za wachezaji kiafya zinaendelea vema na anashukuru hadi sasa hana majeruhi yoyote.

"Hakuna mchezaji ambaye ni majeruhi hadi sasa, na ninashukuru kwa hilo, kikubwa ni kupata matokeo mazuri katika mchezo huo," aliongeza.

Alisema wiki ijayo wanatarajia kuanza safari kuelekea Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo.

Namungo kwa sasa inashikilia nafasi ya 6 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 36 baada ya mechi 27.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Arama Benoit, akishiriki mbio za kilometa tano katika mashindano ya Tulia Marathoni yaliyofanyika Mbeya, kwa lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu. Kampuni ya Oryx Gas ilikuwa mdhamini mwenza katika mashindano hayo ukiwa ni msimu wa saba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Yanga yashusha presha kwa Marumo

INATOKA UK. 24

wapinzani siyo wabaya na hatupaswi kuwadharau kutokana na nafasi waliyopo kwenye ligi ya kwao, kwa sababu ligi haina mtoano kama hii michuano ya CAF.

"Kikubwa tunaenda kucheza nao tukiwa hatuna presha kwa sababu tunajua tunaenda kucheza na mpinzani wa aina gani na yupo katika wakati gani, lakini tunachoweza kukiangalia upande wetu ni kutafuta matokeo ya ushindi."

Kikosi cha Yanga kinaendelea na mazoezi yao kwenye kambi yao Kigamboni Dar es Salaam kujiandaa na mchezo huo.

## Simba SC hatarini

INATOKA UKURASA 24

kukaa na mpira.

Kuumia kwa Mbombo na kuingia Dube ndiko kulikowaumiza Simba kwani hakuchukua muda mrefu kuweka mpira ndani ya wavu.

Kocha Roberto Oliveira, alilazimika kuwatoa Jean Baleke na Kibu Denis, nafasi zao kuchukuliwa na John Bocco na Pape Sakho, lakini hali ilikuwa ngumu.

Nafasi pekee kubwa iliyoipata Simba ilikuwa ni dakika mbili kabla mechi kumalizika, Bocco alipoachia shuti kali la mbali, lililotemwa na kipa Iddrisu.

Kuna dalili zote za Simba kukosa kila kitu msimu huu, kwani baada ya kutolewa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Wydad Athletic Club ya Casablanca Morocco, Simba haina matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya sare ya bao 1-1 kwenye mechi iliyochezwa Jumatano iliyopita dhidi ya Namungo na sasa imelikosa Kombe la FA.

Azam sasa inasubiri mshindi kati ya Yanga dhidi ya Singida Big Stars kwa ajili ya fainali itakayochezwa Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

Michezo
Jumatatu Mei 8, 2023
Nipashe



‘Wachezaji mnaweza kunywa mvinyo’ UKURASA 21



Mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube (katikati) akishangilia pamoja na wachezaji wenzake baada ya kufunga bao la ushindi dhidi ya Simba kwenye mchezo wa nusu fainali ya kombe la FA jana katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara. Azam ilishinda 2-1 na kutinga fainali. **PICHA: AZAM FC**

## Yanga SC yashusha presha kwa Marumo

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, ameitoa kauli ya kibabe kwa kusema kuwa hawana wasiwasi tena juu ya wapinzani wao katika hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), Marumo Gallants ya Afrika Kusini baada ya kupata muda wa kutosha kuwaangalia katika mchezo wao dhidi ya Mamelod Sundown.

Yanga inajiandaa kucheza na Marumo keshokutwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kurudiana Mei 17, mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Marumo kwa sasa wanapambana kubakia katika Ligi Kuu ya Afrika Kusini kutokana na kuwa kwenye hatari wa kushuka daraja licha ya kufanya vizuri kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ambapo juzi Jumamosi ilikubali kichapo cha mabao 2- 0 kutoka kwa Mamelod katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Thohoyandou.

Akizungumza na Nipashe jana Kaze alisema wamepata muda wa kutosha wa kuwasoma wapinzani wao hao kuelekea katika mchezo wao, hali inayowapa matumaini makubwa ya kuweza kufanikiwa kupata ushindi wa kwenda katika hatua ya fainali ya michuano hiyo.

Alisema wamewaona wapinzani wao na kuona ubora na udhaifu wao na wana nafasi kubwa ya kumaliza mchezo kwenye Uwanja wa Mkapa, kwa sababu wamepata muda wa kuwaangalia katika mchezo wao mkubwa wa ligi juzi.

“Tumepata muda wa kuangalia mechi yao na walipoteza, hii imetusaidia kupunguza presha, lakini tumeweza kuona mapungufu yao yapo katika nafasi zipi ambazo zinaweza kutusaidia kupata ushindi,” alisema Kaze.

Aliongeza: “Ukweli

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba hatarini kutoka kapa

## Ni baada ya kutolewa nusu fainali ya FA, huku matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu yaki...

**Na Adam Fungamwangwo**

AZAM FC imekuwa timu ya kwanza kutinga hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (FA), baada ya kuiadhibu Simba mabao 2-1 kwenye mechi kali ya nusu fainali iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.

**Alikuwa ni yule yule, Prince Dube ambaye amekuwa akiwafunga mara zote msimu huu kwenye Ligi Kuu, akiwafunga tena kwenye mechi ya Kombe la FA.**

Dube aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Idris Mbombo, alipachika bao la pili dakika ya 76 baada ya uzembe wa mabeki wa Simba kushindwa kukaba mpira na njia.

Ayoub Lyanga ambaye alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu jana, akaupiga mpira kichwa na Dube akakimbia akifukuzana na mabeki kwenye wingi ya kulia na kuupiga kiufundi kwa juu, mpira huo ukakatika na kujaa wavuni, ukiwaacha walinzi na kipa wao Ally Salim hawana la kufanya.

Straika huyo aliyewatanguliza Azam kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga kwenye fainali ya kombe hilo, aliifunga Simba bao kwenye mechi ya Ligi Kuu mzunguko wa kwanza Oktoba 27 mwaka jana, akafunga tena bao pekee dakika ya 35, Azam ikishinda 1-0, na mechi ya mzunguko wa pili iliyochezwa Februari 21, mwaka huu alipachika bao sekunde ya 15, mechi ambayo timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

Kiungo mkabaji Sadio Kanoute ambaye aliipatia Simba bao la kufutia machozi, alioneshwa kadi nyekundu dakika nne kabla ya mechi kumalizika na mwamuzi Tatu Malongo kutoka Tanga kwa kumchezea madhambi James Akaminko wakati tayari ana kadi ya njano.

Katika mchezo huo, Simba ilianza mapema kulitia msukosuko lango la Azam kwenye dakika ya tatu tu ya mchezo, baada ya faulo ya Clatous Chama iliyokuwa ikielekea wavuni kupanguliwa na kipa Iddrisu Abdulai na kusababisha purukushani kwenye lango, lakini mabeki wakafanikiwa kufagia hatari hiyo.

Kosa lililofanywa na Joash Onyango dakika ya 11, kuukosa mpira wa kichwa, ulimpa nafasi Idris Mbombo kuuchukua pembeni kidogo mwa uwanja na kupiga krosi iliyoleta kizaazaa kwenye lango la Simba, kabla haujatolewa na kuwa kona.

Kona hiyo iliyopigwa dakika hiyo hiyo, nusura izae bao, kwani uliunganishwa kichwa na Mbombo, mpira ukagonga nguzo ya pembeni na Mohamed Hussein 'Tshabalala' akauondoa kwenye hatari.

Shuti kali la Kanoute lilikwenda nje kidogo ya lango dakika ya 16, alipomegewa pande safi kutoka kwa Saido Ntibazonkiza.

Baada ya kosakosa nyingi, hatimaye Azam iliandika bao la kwanza dakika ya 23 lililowekwa wavuni na beki wa kulia, Lusajo Mwaikenda kwa shuti kali la karibu, akiufumua mpira uliotemwa na kipa Ally Salim.

Ulikuwa ni mpira wa faulo iliyopigwa na Ayoub Lyanga, baada ya kufanyiwa madhambi na Shomari Kapombe, shuti lake lilitemwa na kipa Salim, lisababisha patashika nguo kuchanika langoni, kabla ya mfungaji kuukwamisha wavuni.

Simba ilisawazisha bao hilo dakika tano baadaye, Kanoute akiruka juu kuliko mabeki na kipa wa Azam, akaukwamishwa mpira wavuni kwa kichwa.

Aliunganisha mpira wa faulo uliopigwa na Ntibanzonkiza, kutokana na Kibu Denis kufanyiwa madhambi na Brice Kangwa.

Chama alikosa mabao mawili, dakika ya 32 na 45 ambayo kama angetumia nafasi vizuri, Simba ingeweza kwenda mapumziko ikiwa na mabao matatu.

Kipindi cha pili, Azam iliingia tofauti na kuutawala mchezo kwa kiasi kikubwa na kuwanyima nafasi wachezaji wa Simba

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >